SUPA JACKPOT
TZS.1,090,583,531
KWA TZS. 1000 TU!
SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!
SportPesa.CO.TZ
PIGA *150*87#



UKURASA 4

**MIAKA MIWILI IKULU**
Alivyopambana na UVIKO-19, kuzuia Ebola kuingia nchini


Nipashe TESA
Jumanne Machi 14, 2023
TEKNOLOJIA • ELIMU • SAYANSI
MIAKA 2 RAIS SAMIA Anavyowatoa gizani 1,600 waliokwama kusoma ni wa sekondari, takwimu za msingi zaandaliwa
Ushoga na ndoa za jinsia moja unavyopingana na maumbile
ELIMU
NA CHRISTINA MWAKANGALE
Mabinti sikilizeni somo la aliyenusurika ndoa utotoni
•Anawakumbusha semeni 'no' kwenye kuonewa

UKURASA 11


# Nipashe

Jumanne Machi 14, 2023 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0581249

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US


# Masharti mapya bima afya yaanza

**VIFURUSHI** vipya vyaanikwa, hakuna mwanafunzi kukatiwa kama mzazi wake hana... *Endelea ukurasa wa 2*



Mkurugenzi Mtendaji wa ATCL, Mhandisi Ladislaus Matindi, akiongoza kikao na viongozi wa Shirika la Ndege la Senegal kujadili namna ya kukabiliana na changamoto za msingi za ndege za Airbus A220-300 kilichofanyika jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

**KUBAINIKA NDEGE MBOVU**

## ATCL na Air Senegal waungana kuwajibisha watengeneza Airbus

UKURASA 2

## Saba wafariki dunia kwa madai ya kula samaki wenye sumu

UKURASA 3

**MICHEZO** FEI TOTO AITWA STARS MECHI KUFUZU AFCON UK. 24

**KATUNI** UK. 6

# Masharti mapya bima afya yaanza

**Na Christina Mwakangale**

UONGOZI wa Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF) umesema watumiaji wa mfuko huo waliomo kwenye kundi la watoto, wakiwamo wanafunzi wa shule za msingi, sekondari na elimu ya juu, ambao walikuwa kwenye kifurushi maalum kwa kulipia Sh. 50,400 kwa mwaka, sasa hawatatumia utaratibu huo.

Mfuko huo sasa una utaratibu mpya ulioanza jana Machi 13, kundi hilo linalazimika kulipiwa malipo yao kupitia uanachama wa wazazi au walezi wao ambao ni wanachama kupitia vifurushi vya mfuko kulingana na ukubwa wa familia.

Vifurushi hivyo ni vilivyopewa majina ya Najali Afya, Timiza Afya na Wekeza Afya.

Januari mwaka huu, Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu, alisema atasimama kidete kuhakikisha kila Mtanzania anafahamu umuhimu wa kuwekeza na kuweka kipaumbele kwenye afya na hakutakuwa na msamaha wowote.

Waziri Ummy alisema ajenda kuu iliyopo mbele ya sekta hiyo ni huduma bora na Bima ya Afya kwa Wote, ambayo kwa sasa kiwango kinachotazamiwa ni kuwa kati ya Sh. 340,000 hadi 360,000 kwa mwaka, ili kuhudumia watu sita kwa huduma za rufani, kanda na kibingwa.

**UTARATIBU MPYA**

Meneja Uhusiano wa NHIF, Angela Mziray, jana aliiambia Nipashe iliyotaka kufahamu utaratibu mpya kuhusu huduma hizo, kwamba ulianza rasmi jana na bei za vifurushi kulingana na familia za wachangiaji kuanzia umri wa miaka 18 hadi 35, ni kuanzia Sh. 192,000 kwa huduma za kifurushi cha Najali Afya; Sh. 384,000 (Wekeza Afya) na Sh. 516,000 kwa Timiza Afya.

Aidha, kifurushi kama hicho yaani mtu mmoja, bila wategemezi, kwa wachangiaji kuanzia umri wa miaka 35 hadi 59 gharama ni Sh. 240,000 kwa huduma za kifurushi cha Najali Afya; Sh. 444,000 (Wekeza Afya) na Sh. 612,000 kwa Timiza Afya.

Kadhalika, vifurushi kwa ajili ya wanandoa pamoja na mtoto mmoja kwa wachangiaji kuanzia umri wa miaka 18 hadi 35, ni Sh. 504,000 kwa kifurushi cha Najali Afya; Sh. 924,000 (Wekeza Afya) na Sh. 1,272,000 kwa kifurushi cha Timiza Afya.

Pia kifurushi kwa ajili ya wachangiaji kuanzia umri wa miaka 36 hadi 59 wakijumuishwa watoto wawili, gharama ni Sh. 696,000 (Najali Afya); Sh. 1,248,000 (Wekeza Afya); Sh. 1,728,000 (Timiza Afya) kwa mwaka.

"Ni kweli kuna utaratibu mpya na maboresho kuhusu usajili wa watoto. Watoto walikuwa wanaweza wakaingia kama watoto wenyewe, maboresho yaliyofanywa sasa hivi, wanahitaji watu waingie kama familia, kaya au kupitia shule zao.

"Sio awali ilikuwa mtoto mmoja, ilikuwa na changamoto na malalamiko mengi ikiwamo kupita miezi mitatu ili uanze kuhudumiwa, utakuta mtoto anakuja anasajiliwa, lakini mzazi wake sio mwanachama, au utaratibu wa kishule, waingie kama shule," alisema.

Angela alisema utaratibu huo unawagusa wanachama wa mfuko huo ambao malipo yao yamefikia kikomo na kwamba wakitaka ku-renew (kupitia) bima hizo, wajiunge kupitia utaratibu wa familia, kaya au wazazi wao ambao wanahudumiwa na kampuni au taasisi fulani.

"Sasa hawa watasajiliwa kama kaya, makundi au shule zao. Msingi, sekondari kama ilivyokuwa kwa vyuo huja kama chuo wakiwasajili. Utakuta mzazi hana bima, ila anasubiri mtoto akiumwa ndipo amsajili mtoto wake, hii ni risk (hatari)," alisema Angela.

Kwa utaratibu huo, Angela alisema matarajio ni kundi kubwa la watu kujisajili kupitia vifurushi na kwa kipindi cha mwezi mmoja, waliojiunga kama shule, familia au vikundi watakuwa wanaanza kuhudumiwa na mfuko huo tofauti na awali, ikiwapasa kusubiri miezi mitatu.

"Vifurushi mama anaweza akaingia na mtoto mmoja, au baba na watoto wawili. Kujisajili sasa itabidi shule zisajili watoto wao, wazazi waamue utaratibu huu na shule wajiunge na kuwa na kundi la wanafunzi. Usajili utapitia shule, ingawa tutaangalia baadaye kama utasuasua," aliongeza.

Angela alisema kwa wanachama wa vikundi ikiwamo vya umoja wa tasnia tofauti, ikiwamo waandishi wa habari, ambao kila mwanachama alilipia Sh. 100,000 kwa mwaka, mazungumzo yanaendelea na iwapo kutafanyika maboresho, yatawekwa hadharani.

**MAONI WANACHAMA**

Baadhi ya wazazi, walezi na watumiaji wa huduma za NHIF, wakizungumza na Nipashe jana, walisema hatua ya serikali kusitisha utaratibu wa kulipia upya (renew) bima za watoto waliopo, uangaliwe kwa umakini kwa kuwa unaweza kusababisha mtoto kukosa huduma ya matibabu kutokana na kukosa fedha taslimu ya kulipia.

Denis Brighton alisema ni kawaida kufanya malipo ya bima ya afya ya mwanawe kila mwaka, akisema kila mwaka huduma hiyo inapokaribia kufikia ukomo hupewa taarifa na mfuko huo ya kutakiwa kulipia.

"Nimetumiwa taarifa na NHIF na ujumbe ni huu mwandishi, unanieleza nifike ofisi za bima ya afya ku-renew (kuhuisha) uanachama kwa kulipia Sh. 50,400 kwa ajili ya bima ya mtoto wangu, ninafika hapa ninaambiwa siwezi kurenew, unakuja utaratibu mpya.

"Kinachonishtua bima hii ni ya mtoto. Je, akiumwa inakuwaje? Wakanijibu nitalipia fedha cash (taslimu). Kadi ya bima ya mtoto wangu inaonyesha inatumika miaka mitano, yaani itaisha mwaka 2026 na kwa mfumo wa kulipia kila mwaka," alisema Denis.

Agnes Magwa alisema utaratibu huo unaweza kuwa mzuri ingawa kwa sasa tatizo lipo katika maandalizi, ili mzazi kumudu gharama ya vifushi hivyo kwa mwaka."Ilikuwa Sh. 50,400 tu ninamlipia mtoto mmoja, nilimudu kila mwaka, nilikuwa nipo radhi mimi nisijilipie huduma ya mfuko, ila angalau niwe na uhakika wa mtoto wangu kutibiwa," alisema Agnes.

**WAZIRI**

Waziri wa Afya, Ummy, akizungumza hivi karibuni, alisema mfuko huo unaelemewa kutokana na kulipia gharama kubwa kwa ajili ya magonjwa yasiyoambukiza (NCD), miongoni mwake ni kisukari, kiharusi na shinikizo la juu la damu, ikifahamika zaidi kwa jina la presha.



Alisema magonjwa hayo yameugharimu mfuko takribani Sh. billioni 99.09 kwa kipindi cha mwaka 2021/22 na hali hiyo inahatarisha mfuko, akisema njia pekee kwa jamii ni kupatiwa elimu kuepukana na magonjwa hayo.

Alibainisha NHIF inatoa huduma kwa wanachama milioni 4.33, sawa na asilimia nane ya Watanzania wote wapatao milioni 60, huku asilimia sita wakihudumiwa na Mfuko wa Afya ya Jamii (CHF).

## ATCL, Air Senegal kuwachukulia hatua watengeneza ndege

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya Ndege Tanzania (ATCL) iko katika mazungumzo ya awali na Shirika la Ndege la Senegal (Air Senegal), kuangalia uwezekano wa kuwawajibisha watengenezaji wa ndege aina ya Airbus, wanazodai zina upungufu wa aina tatu walioubaini, taarifa rasmi imeeleza.

Madai hayo yanatajwa katika sehemu kuu tatu; udhaifu wa injini, kupata kutu mapema na bodi ya ndege hizo hazikidhi viwango, hali inayofanya vyombo hivyo vya usafiri kulazimika kusimama kila mara pasi na kufanya kazi.

Taarifa ya Kitengo cha Uhusiano kwa Umma cha ATCL jana, ilimnukuu Mkurugenzi Mtendaji wa kampuni hiyo, Mhandisi Ladislaus Matindi akitamka tatizo hilo limethibitika kwenye ndege kubwa aina ya Airbus A220-300, hali iliyodhihirika hata kwa ndege kama hizo kwingineko duniani.

Hadi sasa inaelezwa barani Aftrika, kampuni hizo mbili na nyingine la Misri, Egypt Air, ndizo zinatumia aina hizo za ndege katika huduma zake za usafiri wa anga.

Kwa mujibu wa Mhandisi Matindi, wakati changamoto ya kutu kulingana na mwongozo wa matengenezo yake inapaswa kujitokeza baada ya miaka saba, lakini kwa ndege hizo ilijitokeza ndani ya miaka miwili na miezi miwili, huku ndege hizo hadi sasa zimeshatumika kwa miaka mitatu kasoro mwezi mmoja pekee, yaani miezi 35.

Aidha, kuhusu changamoto ya kutu, inaelezwa iligundulika muda mfupi baada ya kupokelewa ndege hizo. Mhandisi Matindi alitaja mfano wa ndege yenye namba 5H-TCI ilipata kutu ikiwa na wastani umri wa miezi 26 pamoja na 5H-TCH, wastani wa umri wa miezi 35, baada ya kuanza kufanya kazi nchini.

Mhandisi Matindi alifafanua, kwa mujibu wa mwongozo wa matengenezo ya ndege hizo (Maintenance Planning Document - MPD), tatizo la kutu lingeanza kuonekana baada ya miaka saba ya matumizi yake, lakini injini zimeanza kufanyiwa matengenezo mapema, ikiwa ni asilimia 19 ya matumizi ya ndege hizo, kabla ya kutimu wakati sahihi kufanyiwa matengenezo.

"Injini aina ya PW1524G-3 zinazotengenezwa na Pratt and Whitney (PW) zilizofungwa kwenye ndege za A220-300, zinapaswa kutolewa kwa matengenezo zikiwa zimefikisha muda wa miruko (landings) 5,260, lakini kutokana na upungufu wa uundwaji wa injini hizo (design), zimelazimika kutolewa kabla ya muda pangwa, injini zikifikia miruko 1,000 tu".

Alifafanua kwamba, aina hiyo ya ndege ina hitilafu ya injini, huku kukiwa na upungufu mkubwa wa injini mbadala, hali inayolazimu ndege kusimama kwa muda mrefu kusubiri matengenezo, hata kusababisha kuathirika ratiba za ATCL kila mara, sambamba na mapato yake.

Mkuu huyo wa ATCL alisema, tatizo la kutu alilolitaja sasa linachangia shirika kubeba mzigo wa gharama za uendeshaji, ihali iliyogundulika muda mfupi baada ya kupokewa ndege hizo, ikimaanisha kampuni imekuwa ikibeba gharama za ziada muda wote.

Mhandisi Matindi alitoa mfano kwamba, ndege yenye namba 5H-TCI ilipata kutu ikiwa na wastani wa umri wa miezi 26 huku yenye 5H-TCH ilibainika kuwa na shida hiyo katika umri wa miezi 35 baada ya kuanza kufanya kazi nchini.

Mwongozo wa kiufundi wa ndege hizo, unaeleza kwamba tatizo la kutu linapaswa kuanza kujitokeza ndani ya kipindi si chini ya miaka saba ya matumizi yake.

**AIR SENEGAL**

Kufuatia changamoto zinazoyakabili mashirika ya ndege yanayotumia ndege aina ya Airbus A220-300, viongozi wa juu wa Air Senegal wametembelea ATCL ili kuangalia namna ya kushughulikia changamoto hizo kwa pamoja.

Akizungumza wakati wa ziara hiyo, Mkurugenzi wa Utawala na Uendeshaji wa Air Senegal, Hanne Samba Sall, alisema wameamua kufanya ziara ya kimkakati nchini ili kubadilishana mawazo na ATCL namna ya kukabiliana na changamoto za msingi za ndege za Airbus A220-300 zinazoathiri uendeshaji wa mashirika yote duniani yanayotumia ndege za aina hiyo.

Samba Sall alidai: "Kampuni ya Pratt and Whitney (PW) ambayo ni mtengenezaji wa injini zinazotumika kwenye ndege hizo, imeshindwa kumudu jukumu lake la kuhakikisha kuwapo injini za ziada ili kuondoa athari za ubovu wa injini zilizoko wakati zikifanyiwa matengenezo."

Alisema Shirika la Ndege la Senegal linapitia wakati mgumu wa uendeshaji kutokana na kukosekana kwa ndege za Airbus A220-300 kwenye mtandao wake wa safari kunakosababishwa na hitilafu za injini huku kukiwa hakuna injini za ziada, kama ilivyo kawaida, ili kuhakikisha shirika linaendelea kutoa huduma.

Alisema uamuzi wa kutembelea ATCL unatokana na ukweli kuwa changamoto za ndege za Airbus A220-300 zilizosababishwa kwa kiasi kikubwa na ubovu wa injini zake, zinafanana kwa mashirika yote yanayotumia ndege za aina hiyo katika safari zao.

Ndege aina ya Airbus A220-300 zina uwezo wa kubeba takriban abiria 130 na kwenda masafa ya kati. Kuwapo kwa kasoro hizo za kiufundi kunaathiri uendeshaji wa kampuni za ndege duniani ikiwamo kukosesha mapato muda wote ndege hizo zinapokuwa chini.



Spika wa Bunge ambaye ni Mwenyekiti wa Kundi la Afrika kwenye Umoja wa Mabunge Duniani, Dk. Tulia Ackson, akiteta jambo na Ester Matiko Mbunge wa Tanzania anayewakilisha umoja huo katika Mkutano wa 146 unaoendelea Manama nchini Bahrain. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mashahidi 26, vielelezo 82 kujenga kesi ya kina Kisena

**Na Grace Gurisha**

MASHAHIDI 26 wanatarajiwa kutoa ushahidi katika kesi ya uhujumu uchumi yenye mashtaka 25 inayomkabili aliyekuwa Mkurugenzi wa Kampuni ya Huduma za Usafirishaji wa Mabasi Yaendayo Haraka (UDART), Robert Kisena (47) na wenzake wawili pia vielelezo 82 vitatumika.

Mashahidi hao wanatoka Benki ya NMB, UDART, BRELA, Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) na taasisi zingine ambapo nyaraka zitakazotumika zinatoka taasisi mbalimbali ikiwamo ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG).

Taarifa hiyo ilitolewa jana mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu, Huruma Shaidi wa Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu na Wakili wa Serikali Mkuu, Achiles Mulisa, akisaidiana na Timotheo Mmari na Nickson Hayo baada ya kuwasomea washtakiwa maelezo ya mashahidi 26.

Mulisa alidai katika kesi hiyo watakuwa na mashahidi 26 na vielelezo 82 ambavyo vilitumika katika uchunguzi wa kesi na kuonyesha jinsi Kampuni ya Simon Group Ltd ilivyonunua hisa na pia kuonyesha wanahisa wa kampuni hiyo. Upande wa mashtaka ulifikia hatua ya kuwasomea washtakiwa maelezo ya mashahidi kwa sababu upelelezi wa kesi hiyo umekamilika, hivyo itahamia Mahakama Kuu ya Tanzania, Kitengo cha Rushwa na Uhujumu Uchumi, maarufu Mahakama ya Mafisadi.

Mbali na Kisena ambaye ni Mkurugenzi wa Simon Group Ltd, washtakiwa wengine katika kesi hiyo ya uhujumu uchumi namba 40/2022, ni Mtendaji Mkuu wa Kampuni ya Simon Group Ltd, Charles Newe na mfanyabiashara Kulwa Kisena (34).

Kati ya mashtaka hayo 25, mashtaka 22 ni ya wizi wakiwa wakurugenzi na maofisa wa UDART, shtaka moja ni la kuongoza genge la uhalifu, lingine la kutakatisha fedha Sh. bilioni 4.4 na kuisababishia hasara serikali ya Sh. 4,460,082,311.

# Saba wafariki dunia kwa madai ya kula samaki wenye sumu

**Na Julieth Mkireri,** MAFIA

WATU saba wakazi wa vijiji vya Bweni na Kanga, Wilaya ya Mafia wanadaiwa kupoteza maisha baada ya kula nyama ya samaki aina ya kasa.

Tukio hilo linadaiwa kutokea Machi 12, majira ya saa mbili usiku baada ya kula nyama hiyo.

Akizungumza kwa njia ya simu, Mwenyekiti wa Kijiji cha Bweni, Juma Khatibu, alisema watu hao walikumbwa na umauti baada ya kuuziwa samaki huyo anayedaiwa kuwa na sumu.

Khatibu alisema samaki huyo haruhusiwi kisheria kuliwa na watu, lakini wapo wavuvi wanauza kwa njia za siri.

"Tukio hili lilitokea Machi 11, Jumamosi, hao wavuvi baada ya kuvua samaki huyo walimtengeneza kabisa wakiwa feri na wakawauzia wateja wao kwa njia ya siri, baada ya kula madhara yameanza kuonekana Machi 12 kwa wale wote walionunua," alisema.

Alisema kuwa kata zilizonunua samaki huyo wengine waliwagawia majirani ambao nao wameathirika.

Alisema hadi sasa vifo ni saba huku wagonjwa wanane wakiendelea na matibabu katika hospitali ya wilaya na ya tarafa Kilongwe.

Hata hivyo inadaiwa waliohusika kuuza samaki huyo hadi sasa hawajulikani walipo kwa kuwa baada ya kupata taarifa za madhara yaliyotokea hawajaonekana.

Mmoja wa waliokula samaki huyo, Shida Abdallah, mkazi wa Kijiji cha Bweni alisema waliletewa na jirani yao ambaye alinunua kwa mvuvi.

Shida alisema wamekuwa wakila samaki huyo mara kwa mara, lakini kwa awamu hii ndio imewasababishia madhara.

"Jirani yetu kila akinunua kasa anatuletea tunakula, lakini hatupati madhara, safari hii tulipokula mimi niliumwa tumbo nikaenda kupata matibabu nimepona ila nimeshauriwa nisimnyonyeshe mtoto, yupo mmoja wa mama amefariki pamoja na mwanawe ambaye alikuwa bado ananyonya," alisema.

Diwani wa Kanga eneo lilipotokea tukio hilo, Khatibu Faki, alithibitisha kuwapo na taarifa hizo na kwamba wananchi hao waliokufa kwa kula samaki aina ya kasa anayedhaniwa kuwa na sumu.

Kwa mujibu wa Diwani huyo kati ya vifo saba watoto ni sita.

Katibu Tawala Wilaya ya Mafia, Gilbert Sandagila, alikiri kuwapo kwa taarifa hizo ambaye alisema ukweli kuhusiana na chanzo cha tukio wanaendelea kufuatilia.

# Japan kusaidia milioni 943/- kubadili sura shule Bara, Z'bar

**Na Maulid Mmbaga**

SERIKALI ya Japan inatarajia kutoa msaada wa Dola za Kimarenai 407,061 (Sh. milioni 943) kwa ajili ya kutekeleza mradi wa uboreshaji wa miundombinu katika shule Bara na Visiwani ikiwa ni mwendelezo wa ajenda yake ya Usaidizi wa Ruzuku kwa Wananchi kupitia Miradi ya Usalama wa Binadamu (GGHSP).

Hayo yalibainishwa jana mkoani Dar es Salaam na Balozi wa Japan nchini, Misawa Yasushi, wakati wa hafla ya utiaji saini ya msaada huo kati yake na wawakilishi wa halmashauri zinazotarajia kupokea msaada huo kesho, zikiwamo Manispaa ya Kinondoni, Wilaya ya Kusini Unguja, Magharibi 'A' na Jiji la Mbeya.

Balozi Yasushi, alisema serikali ya Japan imekuwa ikitoa msaada kwa jamii ya Watanzania katika sekta mbalimbali zikiwamo afya, elimu na usambazaji wa maji chini ya mpango wa GGHSP tangu 1991.

"Kesho Machi 15, Serikali ya Japan kupitia mpango wa usaidizi wa ruzuku katika miradi ya usalama wa binadamu GGHSP, itaongeza msaada wa ruzuku hadi dola 407,061, takribani Sh. milioni 943, kwa ajili ya utekelezaji wa mradi wa uboreshaji wa mazingira na usafi katika Shule ya Sekondari Mzimuni iliyoko Kinondoni, ambao itagharimu Dola 98,258," alisema.

Alisema kuwa mradi wa pili ni ujenzi wa kitalu cha kale cha taaluma katika Shule ya Msingi Kizimkazi Kusini, Wilaya ya Unguja na utagharimu takribani Dola 123,259 ambayo ni zaidi ya Sh. milioni 286.2.

Mradi wa tatu ni uboreshaji wa usafi wa mazingira katika shule za msingi za Magharibi A katika mkoa wa Mjini Mgharibi Unguja, ambao utagharimu Dola 108,717 sawa na Sh. milioni 252.5.

Wa nne ni uboreshaji wa usafi wa mazingira katika Shule ya Sekondari Lomba mkoani Mbeya, ambao utagharimu Dola 76,827, sawa na Sh. milioni 178.4.

Miradi yote inalenga kuboresha miundombinu ya vyoo iliyochakaa pamoja na kusogeza karibu na shule huduma ya majisafi na salama ili kuweka mazingira rafiki kwa wanafunzi kujisomea.


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, NA UCHUKUZI**

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Barua Pepe:@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Mtumba,
S.L.P. 2888,
DODOMA,
14.03.2023

**TAARIFA KWA UMMA**

1. Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi (Sekta Ujenzi) inapenda kuutaarifu umma kuwa siku ya Alhamisi tarehe **16-03-2023** kampuni ya **Spedag Interfreight Ltd** itasafirisha Mzigo wenye vipimo vikubwa kutoka **Mzenga** kuelekea **Bandari ya Dar -Es-Salaam kupitia Mlandizi** gari hiyo ina namba ya usajili: **NRB 69149 / NRB 43293**

2. Gari hiyo ina vipimo vifuatavyo:
   **Urefu** - **mita 36.00**
   **Upana** - **mita 4.30**
   **Kimo** - **mita 4.60**

3. Njia itakayotumika: **Mzenga, hadi Dar -Es-Salaam kupitia Mlandizi** gari itasafiri muda wa mchana tu ***(Kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12:00 Jioni)***

***Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.***

MAKALA MAALUM

MIAKA 2 SAMIA IKULU

# Afanikiwa kupambana Uviko-19, kudhibiti ebola

Na Mary Geofrey



KIPINDI cha miaka miwili cha Rais Samia Suluhu Hassan kimekuwa cha majaribu mazito kwa sekta ya afya kutokana na ugonjwa wa UVIKO-19 na tishio la Ebola, hali iliyoifanya sekta hiyo kubadili vipaumbele vyake kukabiliana na hali hiyo.

Rais Samia ndiye aliyeruhusu watu kuanza kuchanjwa chanjo ya ugonjwa huo kwa kuchanja na uvaaji wa barakoa hadharani kwenye mikusanyiko, huku watu wakiujadili bila hofu yoyote.

Kabla ya kutangazwa na Shirika la Afya Ulimwenguni (WHO) kuwa ugonjwa huo umekwisha, Tanzania ilichukua hatua madhubuti za kukonga watu wake, ikiwa ni pamoja na kuomba mkopo wa masharti nafuu uliosaidia kukuza sekta mbalimbali zilizoathiriwa na ugonjwa huo.

Chanjo na uvaaji wa barakoa ulisaidia watu wengi kutopoteza maisha na kuondoa hofu kubwa iliyokuwapo iliyotishia uhai wa watu baada ya Rais Samia kuwa mstari wa mbele kukabiliana nao.

Alihakikisha chanjo za kutosha zinaingia nchini na kuwa na kampeni ya kuchanja kila Mtanzania, ikiwa ni pamoja na kutoa elimu kwa umma juu ya umuhimu wa kuchanja.

Kutokana na jitihada hizo Shirika la Fedha Ulimwenguni (IMF), liliishinisha mkopo wa Sh. trilioni 1.3 kwa ajili ya kuboresha sekta ya afya, maji, elimu na miundombonu, lengo likiwa ni kuboresha upatikanaji wa huduma za afya na sasa kuna vituo na zahanati hadi ngazi ya chini.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na Wizara ya Afya hadi Desemba 2022, watu 29,123,387 walichanja sawa na asilimia 94.7 ya lengo la watu 30,740,924 na kwamba Tanzania ilipokea dozi 24,376,529 ambazo zimesambazwa nchini.

**BIMA YA AFYA**

Bima ya Afya kwa wote ni moja ya mambo makubwa yanayopigiwa chapuo na Rais Samia, kuhakikisha inaleta mafanikio kwa maslahi mapana ya taifa na kuutangazia umma utayari wa serikali yake kuhakikisha kila Mtanzania ana uhakika wa matibabu.

"Sheria za bima ya afya zilizopo kwa sasa, hazijajumuisha makundi yote ya wananchi katika mfumo na hivyo kuacha kundi kubwa la wananchi sawa na asilimia 85 nje ya mfumo wa bima ya afya," anasema Waziri Afya, Ummy Mwalimu.

Anasema hadi mwisho wa mwaka 2021, kati ya Watanzania wanaokadiriwa kufikia milioni 57.7 ni wananchi milioni 8.5 sawa na asilimia 15 ya wote ndio wanaonufaika na mfumo wa huduma za bima ya afya.

Serikali ilianza hatua za awali za maandalizi ya kutunga Sheria ya Bima ya Afya kwa wote tangu mwaka 2012 na baada ya miaka 10 ya majadiliano na makundi mbalimbali, imekamilisha rasimu ya Muswada wa Sheria ya Bima ya Afya na imewasilisha Bunge na kusomwa kwa mara ya kwanza katika mkutano wa nane.

Muswada huo ambao ulikuwa uwasilishwe bungeni kwa mara ya pili Februari 9, 2023 jijini Dodoma ulikwama na sasa utawasilishwa kwenye Bunge la Aprili.

**VIFAA TIBA, DAWA**

Waziri Ummy anasema chini ya uongozi wa Rais Samia kuna ongezeko la idadi ya vituo vya kutolea huduma za afya kutoka 6,871 mwaka 2015/16 hadi kufikia 10,380 mwaka 2021/22.

Watumishi wa sekta hiyo wameongezeka kutoka 86,152 mwaka 2015/16 hadi 102,469 mwaka 2021/22 na bajeti ya dawa na vitendanishi imeongezeka kutoka Sh. bilioni 30 mwaka 2015/16 hadi kufikia Sh. bilioni 230 mwaka 2022/23.

Aidha, ili kuimarisha na kusogeza upatikanaji wa huduma za vipimo vya kibingwa ngazi ya mikoa, serikali inaendelea kusambaza na kusimika mashine za kisasa za CT-Scan katika hospitali ngazi ya Taifa, Kanda na hospitali za rufani za mikoa 28.

Katika kuimarisha upatikanaji, usambazaji na utunzaji wa dawa, serikali imefanya maboresho makubwa katika uongozi wa Bohari Kuu ya Dawa (MSD) kwa lengo la kuongeza tija na ufanisi.

"Pamoja na juhudi zilizofanywa na serikali za kuimarisha upatikanaji na utoaji huduma za afya nchini, bado kumekuwapo changamoto kwa baadhi ya wananchi kushindwa kugharamia uchangiaji wa huduma za afya pindi wanapougua na wakawa hawana fedha," anasema Ummy.

**KUDHIBITI EBOLA**

Septemba 20, 2022, serikali ilipata taarifa ya mlipuko wa ugonjwa wa ebola katika Wilaya ya Mubende nchini Uganda, udhibiti ulifanyika kwenye mipaka na kutoa elimu kwa umma.

Ugonjwa huo uliendelea kusambaa na kufikia wilaya 10 ikiwamo Jiji la Kampala na Entebbe na hadi kufikia Oktoba 31, 2022 jumla ya wagonjwa 130 walithibitika kuwa na ugonjwa huo na 43 kufariki. Serikali imefanikiwa kudhibiti ugonjwa huo kutoingia nchini.

**UFADHILI WA MASOMO**

Katika kipindi cha mwaka 2023, serikali imetoa ya watumishi 457 kupata ufadhili na kati yao 318 wamechaguliwa katika utaratibu wa kawaida na watumishi 139 wamepata katika utaratibu mpya wa mafunzo ya kimkakati kwa utaratibu wa set.

Ufadhili huo unatambulika kama Mpango wa Samia wa kuongeza wataalamu Bingwa na Bobezi wa Afya nchini.

Ufadhili huo ni kwa ajili ya malipo ya ada kwa asilimia 100 kwa chuo husika na posho ya utafiti kwa waliopata ufadhili kwa vyuo vya ndani ya nchi.

Kwa wanaofadhiliwa nje ya nchi watalipiwa ada kwa asilimia 100, ikiwamo posho ya utafiti, nauli pamoja na posho ya kujikimu wakiwa masomoni. Kwa wale walioomba ufadhili maalumu watagharamiwa kama walivyoomba.

Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi ya Tiba ya Mifupa, Ubongo na Mishipa ya Fahamu, Dk. Respicious Boniface, anasema kuwapo kwa ufadhili huo wa masomo kwa madaktari na watoa huduma za afya nchini, kunawajengea uzoefu wataalamu hao kutoa huduma za kibingwa ambazo wagonjwa walikuwa wanazifuata nje ya nchini.

**MABINGWA WABOBEZI**

Katika kuhakikisha vituo vya kutolea huduma za afya vinawatumishi wenye weledi na ujuzi wa hali ya juu, Wizara ya Afya ilijiwekea lengo la miaka mitano (2020-25) la kusomesha wataalamu bingwa na bobezi wasiopungua 300 kwa kila mwaka wa fedha.

Katika utekelezaji wa mpango huo kwa kipindi cha miaka miwili (2020/21 na 2021/22) wizara imefanikiwa kusomesha wataalamu bingwa 524 ambao wanaendelea na masomo kwenye vyuo mbalimbali ndani na nje ya nchi.

Hadi kufikia Desemba 2021, mahitaji ya wataalamu bingwa katika hospitali zinazotoa huduma za kibingwa na kibobezi nchini yalikuwa 1,782 wakati huo ilikuwa imeshawasomesha wataalamu 992 wa fani mbalimbali za kibingwa na kibobezi.

Hatua hii imewezesha uboreshaji wa huduma za afya za kibingwa na bobezi katika hospitali mbalimbali nchini hali inayochangia kuimarika kwa huduma za matibabu nchini na hivyo, idadi ya wagonjwa wanaopata rufaa ya matibabu nje ya nchi imekuwa ikipungua mwaka hadi mwaka.

Mfano katika kipindi cha mwaka 2014/15 (wagonjwa 683), 2015/16 (wagonjwa 385), 2020/21 (wagonjwa 56) na hadi kufikia Machi 2021/22 jumla ya wagonjwa walikuwa 37.

Kwa mwaka wa fedha 2022/23 serikali imeongeza fedha za kusomesha wataalamu bingwa na bobezi hadi kufikia Sh. bilioni 8 kutoka Sh. bilioni 3 za mwaka wa fedha 2021/22.

Watumishi hao wanapochaguliwa kwenda kusoma wanakuwa kwenye seti ya wataalamu wa fani mbalimbali watakaokamilisha huduma husika mfano matibabu ya upandikizaji figo (Renal Transplant) na matibabu ya saratani (Oncology).

Mfano, wataalamu watakaosomeshwa kwa ajili ya kutoa huduma ya matibabu ya figo kikamilifu katika seti ni kama ifuatavyo; Daktari Bingwa wa Upasuaji figo, Daktari Bingwa wa matibabu ya figo, Daktari Bingwa wa utoaji dawa ya Usingizi kwa wagonjwa wa figo, Daktari Bingwa wa Mionzi,

Muuguzi Bingwa wa Mionzi, Mteknolojia Mionzi, Muuguzi Bingwa wa figo, Muuguzi Bingwa wa Usimamizi wa huduma za chumba cha upasuaji kwa wagonjwa wa figo na Mtaalamu wa Vifaa Tiba vinavyotumika kwa ajili ya matibabu ya figo.

Kwa mwaka wa fedha 2022/23 kupitia Mpango wa kufadhili watumishi wa afya katika fani za ubingwa na ubobezi, wizara itatoa ufadhili wa mafunzo ya set yaliyowasilishwa na taasisi mbalimbali katika maeneo ya kibobezi na kibingwa kupitia mpango huo na jumla ya watumishi 139 wamechaguliwa kupata ufadhili wa masomo na kati ya hao 136 watasomeshwa nje ya nchi na tatu ndani ya nchi.

Mkurugenzi wa Sera na Mipango wa Wizara ya Afya, Edward Mbaga, anasema madaktari wa Tanzania kwenda kuongeza ujuzi nje ya nchi kunasaidia kuwajengea uwezo wa kutoa huduma za kibingwa nchini.

"Lengo ni kuhakikisha huduma za afya zinawafikia Watanzania na kupatikana kwa uwezo na umahiri mkubwa. Tukio la leo lina utekelezaji wa sera kwa sababu wenzetu wa MOI wakishirikiana na wenzao wa Marekani wameandaa kongamano hili ili kuhakikisha wananchi wanapata huduma za kibingwa hasa za magonjwa yasiyo ya kuambukiza kama uvimbe kwenye ubongo," alisisitiza Mbaga.

Mbaga anasema takwimu zinaonyesha wananchi wengi wanapata huduma za kibingwa nchini, kunakosaidia kupunguza safari za kwenda nje ya nchi kutibiwa ambako mgonjwa mmoja inamgharimu zaidi ya Sh. milioni 30.

# Zelothe ashtukia jengo pacha kujengwa chini ya kiwango

**Na Cynthia Mwilolezi, ARUSHA**

MWENYEKITI wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Mkoa wa Arusha, Zelothe Steven, ameagiza majengo pacha ya mama na mtoto kwenye Kituo cha Afya cha Oldonyosambu, Halmashauri ya Arusha kufanyiwa tathmini kutokana na kujengwa chini ya kiwango.

Pia ameonyesha kukerwa na ubovu wa miundombinu ya barabara za halmashauri hiyo zinazosababisha adha kubwa kwa wananchi wakati wa kupeleka mazao yao sokoni.

Alisema wajumbe wa kamati ya siasa ya mkoa huo, hawaridhishwi na hatua zilizofikiwa za ujenzi wa jengo la mama na mtoto katika kituo hicho cha afya cha Oldonyosambu.

"Wajumbe wa Kamati ya Siasa ya Mkoa wa Arusha hatujaridhishwa kabisa na ujenzi wa jengo la mama na mtoto, katika kituo hiki cha afya cha Oldonyosambu.

"Kwa sababu hiyo ninaagiza iundwe kamati maalum ya kufanya tathmini ya jengo hili, matatizo yatakayobainishwa wahusika wote wachukuliwe hatua mara moja, haiwezekani Rais Samia Suluhu Hassan, ameleta fedha nyingi kwa ajili ya kuwaondolea adha ya matibabu, halafu watu wachache wacheze na fedha hizo."

Kuhusu ubovu wa barabara, amemwagiza Mkurugenzi Mtendaji wa halmashauri hiyo, kuongeza kasi ya ukusanyaji wa mapato ili kuwawezesha kutenga fedha nyingi, kwa ajili ya Wakala wa Barabara za Vijijini (TARURA).

Vilevile, Zelothe, alisema idadi kubwa ya wananchi wanaolima mboga na kufuga mifugo ambayo inalisha Jiji la Arusha wanakabiliwa na tatizo la kupeleka bidhaa zao sokoni, hali inayoathiri uchumi wao.

Alimwagiza Meneja wa TARURA katika Wilaya ya Arumeru, kutimiza majukumu yao ya kazi kwa kutambua barabara zenye changamoto na jinsi ya kuzifanyia kazi licha ya bajeti yao kuwa ndogo.

"Hawa watumushi wa TARURA wakiamka asubuhi sijui huwa wanafanya kazi gani nilitegemea wakiamka asubuhi wafanye kazi ya kukagua barabaraza zilizopo kwenye maeneo yao na kujua changamoto zilizopo ili wazifanyie kazi. Hivi karibuni mvua zitaanza kunyesha sijui wananchi watapita wapi kwa ajili ya kufuata huduma za kijamii na kupeleka mazao yao sokoni," alisema.

Katika hatua nyingine Zelothe alionyesha kutoridhishwa na ukusanyaji wa mapato, pamoja na bajeti waliyotenga ya mwaka wa fedha unaokuja ya Sh. milioni 20 kwa ajili ya TARURA.

"Mkurugenzi bajeti mliyotenga ya shilingi milioni 20 kwa ajili ya TARURA ni ndogo sana, licha ya TARURA kupewa fedha na serikali kuu, lakini ninyi mnatakiwa kuongeza bajeti hiyo," alisema.

Aidha, alisema CCM Mkoa wa Arusha haitakuwa na mzaha katika kusimamia utekelezaji wa miradi ya maendeleo inayotekelezwa kwenye mkoa huo kwa sababu ni chama kikongwe ambacho kimeshika dola kwa miaka mingi na hawataki kupoteza nguvu ya CCM katika kushika dola.

Awali, Meneja wa TARURA Wilaya ya Arumeru, Julius Kaaya, alisema kuwa bajeti ya TARURA ni Sh. bilioni 1.9 na kuhusu barabara ya Mwandeti, mkandarasi alipewa mkataba tangu mwaka jana Novemba, lakini haonekani kwenye eneo lake la kazi na hakueleza sababu za mkandarasi huyo kutoonekana.

Akizungumzia kero ya barabara ya Oldonyosambu-Oldonyowasi, Evaline Mamaida, alisema, barabara hiyo ni mbaya na wanalazimika kukodi pikipiki kwa gharama ya Sh. 1,500 mpaka 10,000 kwa kuomba na wakati wa mvua bodaboda haziwezi kwenda eneo hilo.

# Samsung, Vodacom wajivunia bidhaa mpya soko la Tanzania

**Na Halfan Chusi**

SAMSUNG na Kampuni ya Mawasiliano ya Simu ya Vodacom Tanzania wameshirikiana kwa mara nyingine kuzindua toleo la Samsung Epic Galaxy S23 kwenye duka la kampuni hiyo ya simu lililoko Mlimani City, Dar es Salaam.

Akizungumza wakati wa uzinduzi huo, Mkuu wa Kitengo cha Uzoefu wa Simu za Mkononi Samsung, Mgopelinyi Kiwanga alisema: "Tunafuraha kushirikiana na Vodacom kuleta aina mbalimbali za vifaa vya Epic Galaxy S23 kwenye soko la Tanzania tunapolenga kukua zaidi ukanda wa Afrika Mashariki.

"Tunaamini ushirikiano huu utasaidia sana katika kuongeza ufikiaji wa uendeshaji wa vifaa vyetu na wakati huo huo kujenga uhusiano thabiti na wa kudumu na Vodacom."

Mkuu wa Mauzo na Usambazaji wa Vodacom, George alisema: "Ni kipaumbele chetu kuwa wateja wetu wanakuwa na simu zinazowawezesha kupata mtandao na taarifa ili waweze kufaidi manufaa ya kuunganishwa na huduma zetu.

"Kwa ushirikiano huu, tunakaribisha ingizo hili la simu mahiri sokoni ambalo linakidhi maendeleo ya kiteknolojia kama vile mtandao wa 5G. Kwa kila ununuzi, ninaamini wateja wetu watafurahia uzoefu wa kidigitali watakaojipatia kupitia simu hii."

Alibainisha kuwa simu hiyo (Galaxy S23 Ultra 512 GB) itauzwa kwa Sh. 3,830,000 na toleo la GB 256 litauzwa kwa bei ya chini zaidi na kwamba bidhaa hizo zina dhamana ya miezi 24.

## NOTISI/TANGAZO

**LEGENDS AUCTION MART LTD, DESTENI COMPANY LIMITED, NUTMEG AUCTIONEERS & PROPERTY MANAGERS CO.LTD ,SALEI AUCTION MART LTD,HEDANE ENTERPRISES LTD, MASE INTERNATIONAL LTD,TAUSI AUCTION MART,MASETO AUCTIONEER AND DEBT COLLECTORS, JY AUCTIONEERS CO.LTD, NGOMENI AUCTION MART, REAL MASTER LTD,DRM AUCTIONEERS & CO.LTD, MAS AND ASSOCIATES CO.LTD,MELVA INTERNATIONAL LTD ,YONO AUCTION MART &CO.LTD ,YARDLEY RECOVERIES AUCTION LTD, SUMA JKT AUCTION MART COMPANY LTD,MAJEMBE AUCTION MART LTD, MABUNDA AUCTIONEER MART CO.LTD** kwa mamlaka tuliyopewa na Jamhuri ya Muunganowa Tanzania, chini ya Benki ya **AKIBA COMMERCIAL BANK PLC**, tunatoa notisi ya kulipa deni kwa mdaiwa ndani ya siku 14 kuanzia tangazo hili, Vinginevyo, tutafanya Minada ya hadhara kama ratiba inavyoonyesha.

| TAWI ALILOKOPA | JINA LA MTEJA | AINA YA DHAMANA | JINA LA MWENYE DHAMANA | MAHALI DHAMANA ILIPO | TAREHE YA MNADA |
|---|---|---|---|---|---|
| UBUNGO | FELIX BIRCKMAS ALOYS | NYUMBA YENYE HATI MILIKI NA.175184 KIWANJA NA.1370 KITALU "A" | KASSIAN ANTON NINDI | TABATA KISUKULU | 22/03/2023 SAA 5:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| MBAGALA | MAMU PHARMACY | 1.NYUMBA ILIYOPO KWENYE KIWANJA NA.151,KITALU 'Q10' HATI NAMBA 143195-KIBAMBA 2.NYUMBA YENYE HATI YA MAUZIANO-CHAMAZI DOVYA | AHMAD KASSIM OMARY | 1.KIBAMBA 2.CHAMAZI DOVYA | 28/03/2023 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| UBUNGO | WANSAGULA MOSES NATUMWA | NYUMBA | PILI HARUNA BUHANGWA | PUGU- KINYAMWEZI | 30/03/2023 SAA 5:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| UBUNGO | HAMISI JOHN MBWAMBO | NYUMBA (2) | HAMISI JOHN MBWAMBO | MLANDIZI | 29/03/2023 SAA 5:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| MBAGALA | TRAZIAS ISHENGOMA | NYUMBA | TRAZIAS ISHENGOMA | MBAGALA MWANAMTOTI | 28/03/2023 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| MBAGALA | MBAWALA ACADEMCY | NYUMBA | RAMADHANI JUMANNE MBAWALA | CHAMAZI MSUFINI | 30/03/2023 SAA 5:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| TEGETA | GREENLIVER LIMITED | NYUMBA | LAFAEL ISMAIL HUZILWA | BUNJU "B" | 06/04/2023 SAA 4:30 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| TEGETA | ANGWA CONSTRUCTION CO. LTD | NYUMBA | JASSON ALPHONCE MWAKITWANGE | BUNJU "A" | 06/04/2023 SAA 7:30 MCHANA NA KUENDELEA |
| TEGETA | EDDON MAKALA DAUDI | NYUMBA | EDDON MAKALA DAUDI | KIROMO-BAGAMOYO | 06/04/2023 SAA 4:30 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| TEGETA | SHEILA CLEVELAND NKATA | NYUMBA | SHEILA CLEVELAND NKATA | MBEZI LUIS | 11/04/2023 SAA 4:30 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| TEGETA | VENISA JORAM MBISAMATOLE | NYUMBA | JORAM MBISAMATOLE | TEGETA WAZO | 11/04/2023 SAA 4:30 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| TEGETA | NEEMA STANLEY MOTELWA | NYUMBA | MOHAMED ALLY VUYAA | MAJOHE | 12/04/2023 SAA 4:30 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| TEGETA | ARNOLD CONRAD MTENGA | NYUMBA | ARNOLD CONRAD MTENGA | SALA SALA | 13/04/2023 SAA 4:30 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| TEGETA | SHUKURANI JOSEPHAT MHAWI | NYUMBA | MOHAMED RAMADHANI | MBEZI JUU | 13/04/2023 SAA 4:30 ASUBUHI NA KUENDELEA |

**MASHARTI YA MNADA**

1. Mnunuzi atalazimika kulipa 25% ya bei ya Nyumba, Kiwanja,Gari au Shamba ,papo hapo baada ya mnada kumalizika na 75% itakayobaki italazimika kulipwa ndani ya siku 14
2. Ikiwa mnunuzi atashindwa kutimiza sharti lolote la mnada kuhusiana na malipo ya awali,hatarudishiwa pesa yoyote aliyokwisha ilipa.
3. Kwa mawasiliano zaidi; tupigie simu no.**0714939933/0692836202/0753575752/0787129539**
4. Iwapo ndani ya siku 60 mnunuzi hajakabidhiwa nyumba Benki itarudisha kiasi cha fedha kilichowekwa na mnunuzi Benki bila gharama yeyote.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Tunasubiri tija mkutano Qatar

**MKUTANO** wa mataifa 45 yanayoendelea (LDC's) umemalizika Doha, Qatar, ukiazimia kubadilisha sura ya nchi zinazoendelea ili iwe ya mataifa yenye uchumi imara na maisha bora kwa raia wake.

Tanzania ni moja ya mshiriki wa mkutano huo, lakini aliyeingia na kuondoka akiwa kifua mbele kwa mafanikio yanayopatikana kwenye sekta za kiuchumi na kijamii kwa kipindi cha miaka 10 licha ya kupitia changamoto ya ugonjwa wa UVIKO -19, vita ya Ukraine na athari za mabadiliko ya hali ya hewa.

Akizungumza katika mkutano huo, ulioanza Machi 4 na kumalizika Alhamisi iliyopita, Makamu wa Rais, Dk. Phillip Mpango, anaeleza njia zilizosaidia Tanzania kukua kiuchumi.

Anasema kuwa ni mageuzi ya kisera, kitaasisi na udhibiti yanayolenga kukuza uchumi na kuchochea maendeleo ya sekta binafsi.

Aidha, anataja maendeleo ya viwanda, elimu, afya na miundominu na hasa umeme, reli, bandari na Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA), kuwa ni sehemu ya mageuzi hayo.

Mbinu nyingine ni kuanzisha ubia wa kimkakati wa kikanda, kiserikali na kimataifa na kuongeza ufadhili wa kiuchumi wa masharti nafuu ambapo pamoja na mambo mengine mbinu hizo zimeisaidia nchi kupiga hatua za kimaendeleo na sasa inakaribia kuondoka katika kundi la nchi zenye kipato cha chini.

Anasema uchumi unasalia kuwa thabiti wenye mwelekeo mzuri na kuwa ni moja ya nchi zinazokua kwa kasi kiuchumi kwenye ukanda wa Kusini ya Jangwa la Sahara na zile zilipo katika kundi la mataifa yenye kipato cha chini.

Anataja baadhi ya mafanikio yaliyopatikana kuwa ni kuongezeka kwa maendeleo ya watu kutoka asilimia 0.41 mwaka 2002 hadi 0.55 mwaka jana 2021, umri wa kuishi kupanda kutoka miaka 60 mwaka 2010 hadi miaka 67.2 mwaka 2022, idadi ya watoto chini ya miaka mitano ambao wana utapiamlo (waliodumaa) ilipungua kutoka asilimia 42 mwaka 2010 hadi asilimia 30 mwaka 2022.

Aidha, anataja kiwango cha vifo vya watoto chini ya miaka mitano kupungua kutoka 81 mwaka 2010 hadi 43 kwa kila vizazi hai 1,000 mwaka 2022.

Kadhalika, vifo vya uzazi vimeshuka kutoka 432 mwaka 2015 hadi 250 kwa kila vizazi hai 100,000 mwaka 2021 na maambukizi ya malaria kwa watoto wenye umri wa miezi 6-56 yalipungua kutoka asilimia 18 mwaka 2008 hadi asilimia nane mwaka 2021/22.

Anataja kuondoa ada katika elimu ya msingi na sekondari, kuongeza kiwango cha uandikishaji shule za msingi kutoka asilimia 85 mwaka 2015 hadi asilimia 97 mwaka 2021 ni moja ya mafanikio.

Katika mkutano wa Qatar wa tano wa Umoja wa Mataifa wa Nchi Zinazoendelea za Kipato cha Chini mjadala ulilenga namna ya kukuza uchumi na kuondoka kwenye lindi la umaskini linalokabili mataifa mengi yakiwa ya Afrika.

Mataifa wanachama walijadili utekelezaji wa Mpango wa Utendaji wa Doha (DPoA) ambao umeweka mkazo mambo matano yakiwamo elimu ya chuo kikuu kutolewa kwa mtandao ili kukuza ubora wake, kujenga uwezo na kuhakikisha upatikanaji wa chakula cha kutosha na salama kwa wote, ushirikiano na nchi zinazoendelea kuleta maendeleo.

Tunaamini kuwa baada ya Qatar ni wakati Tanzania kushiriki kikamilifu kufanikisha utekelezaji wa mipango hiyo.

Ili kukabili vikwazo vinavyorudisha nyuma juhudi za kupiga hatua za maendeleo ikiwamo elimu bora, kukosa chakula na kuishi katika hali ngumu na maisha duni yote hayo yakitokana na mfumuko wa bei za vyakula na watu kuwa na uchumi duni.

Tunaona kuwa vijana wengi wanaendelea kukosa ajira, kuwa fukara na hata kukwama kumudu maisha yao, tunashauri uwekezaji zaidi uende kwenye viwanda, biashara, kuongeza thamani kwenye mazao.

Tunashauri pia kufanikisha upatikanaji wa maji karibu kila mahali ni uwekezaji muhimu ili kuwapo na uzalishaji wa chakula na kufuga, lakini kumudu mabadiliko ya hali ya hewa.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677 020 701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Halfani Chusi

# Madanguro haya ni angamizo la taifa

**MEYA** wa Manispaa ya Kinondoni, Songoro Mnyonge, amefichua biashara ya ngono, baada ya kufanya ziara ya kushtukiza kwenye moja ya madanguro yanayotumiwa kwenye ukahaba alipozuru kata ya Makumbusho.

Ziara hiyo ililenga kuangalia namna biashara hiyo ilivyoshika kasi, pamoja na kutafuta mbinu ya kukabiliana na kadhia hiyo.

Baada ya kuona ukubwa wa tatizo hilo, kiongozi huyo anawaagiza wenye nyumba ambao wamewapangisha wanawake wanaouza miili yao, wafike ofisini kwake wakamweleze sababu za kubadili matumizi ya nyumba zao na kuwa madanguro.

Hata hivyo, eneo hilo linapakana na Ofisi ya Mtendaji Kata, na ni njia wanayotumia watoto na wanafunzi kwenda shuleni, hasa wanaosoma shule ya Makumbusho.

Ni jambo linalolalamikiwa na wakazi wa maeneo hayo, wakidai linawaathiri watoto kisaikolojia na kupoteza malengo yao kama anavyoeleza mmoja wa wakazi wa hilo, Juma Ngonyani.

"Watoto wanapita hapa, wanakwenda shule wanaona watu wako utupu, hawana mavazi hivi wanajifunza nini? Kwa vyovyote vile mtoto huyu lazima atamomonyoka kimaadili na usomaji wake utakuwa wa mashaka, akitawaliwa zaidi na fikra za yanayoendelea kwenye madanguro.

"Lakini, wengine tunaishi na familia zetu muda mwingine wazazi kutoka kijijini wanakuja kutusalimia wanapoona hali kama hiyo unadhani wanaondoka na picha gani?" Anahoji Ngonyani.

Aidha, anaioomba serikali kutokomeza biashara hiyo akikumbushia kuwa kama iliweza kuzuia pombe za viroba kitu kilichoonekana kitakuwa kigumu kuzuilika?

Mkazi mwingine wa maeneo hayo, Peter Chikila anasema licha ya 'madadapoa' hao kufanya biashara hiyo wakati mwingine huwaibia wateja wao pale wanapopatiwa huduma na kuongeza changamoto za maisha kwa baadhi ya wanaowahudumia.

"Hapo mnaweza mkapatana kwa bei ya Sh. 2,000 au 3,000, lakini ukishaingia ndani kupata huduma unatakiwa kuwa makini, wakati mwingine anajua mbinu zake za kuongeza buruduni kumbe kwa kufanya hivyo anakuchomolea fedha zako, wengi huwa wanaingia na kutoka wakilia."

Nipashe ilipomtafuta Diwani wa Kata hiyo, Mohamed Ali, anayesema danguro hilo ni la muda mrefu na kwamba amekuwa akilikemea suala hilo bila mafanikio.

"Hili danguro, ni la muda mrefu kwa hiyo tunashukuru manispaa baada ya kupeleka taarifa Meya amekuja kuchukua hatua, ikiwa ni pamoja na kutaka kuonana na wamiliki wa nyumba hizi". Alisema Diwani.

Diwani huyo anasema, biashara hiyo ina madhara makubwa wa kuwa inaweza kusababisha magonjwa kama vile UKIMWI, saratani ya shingo ya kizazi, homa ya ini na maradhi ya kujamiiana hata fangasi za sehemu za siri.

Kuyabaini na kuyafunga madanguro ni juhudi zinazohitaji kuungwa mkono siyo la kuiachia serikali pekee kwa kuwa kizazi kinaangamia na kumomonyoka kimaadili, pamoja na kupotoka kimalezi.

Ni wazi kuwa kinachofanyika kwenye madanguro si uhalifu na uuaji kwa vile wahusika wengi wanaumia kiafya wanaongeza gharama za tiba kwa serikali hasa kwenye sekta ya afya.

Ni kitanzi kwa nguvu kazi ukahaba na uzinzi unaua vijana na Watanzania wenye uwezo wa kufanyakazi. Hivyo hakuna sababu ya kuwa na viwanda vya kuwaambukiza watu maradhi ni lazima kuvikemea.

Ni wazi kuwa wapo vijana wanaosomeshwa na serikali kwa mikopo na kwa gharama kubwa ambao wanashiriki kwenye ukahaba, yote hayo ni hasara kwa taifa na kuendelea kuleta misiba kwa gharama za nchi.

Wasomi wangapi wataangamizwa na madanguro hayo licha ya kusomeshwa kwa mkopo wa elimu ya juu? Ni vijana wangapi watakaoangamia kwa kufunzwa na kulazimika kutumia dawa za kulevya?

Meya anapoulizwa kuhusu madanguro mengine anasema katazo hilo ni kwa madanguro yote ikiwamo lile la Manzese Uwanja wa Fisi, pamoja na Msasani, huku akiwataka wahusika kuachana na biashara hiyo na kujiingiza kwenye ujasiriamali mwingine.

Hili liwe zoezi endelevu na la kudumu kuisafisha Dar es Salaam na Tanzania.

# WMA yatakiwa kubuni mbinu za kiutendaji kuongeza ufanisi

**Na Joseph Mwendapole**

SERIKALI imewataka watumishi wa Wakala wa Vipimo (WMA) kubuni mbinu mpya za kiutendaji zitakazowawezesha kupatikana kwa ufanisi, tija na kufikia malengo ya utoaji wa huduma bora.

Wito huo ulitolewa mwishoni mwa wiki na Katibu Mkuu Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara, Dk. Hashil Abdallah, wakati akizindua Baraza la 32 la Wafanyakazi wa Wakala wa Vipimo lililofanyika jijini Dar es Salaam.

Aliwataka kuondoa vikwazo kwenye uzalishaji kwa kuwezesha biashara kufanyika kwa haki badala ya kuwa watazamaji na kusubiri makosa yafanyike na kuwachukulia hatua wakosaji.

"Tunapaswa kuwezesha biashara kukua, tunapaswa kuwa na sheria, kanuni na taratibu zinazoboresha ufanisi na zinazoboresha mazingira ya biashara. Tusikae ofisini tu kusubiri wakosee tukawape adhabu, ni vizuri kabla hatujawaadhibu tukawaelimisha wafanyabiashara kuhusu makosa yanayoweza kutokea kwa kukiuka sheria na taratibu tulizonazo," alisema.

Kadhalika, aliwapongeza wajumbe wa baraza la wafanyakazi kwa kuaminiwa na kuchaguliwa kuwa wanawakilisha watumishi wengine kwa kuwa uteuzi wao wa kuingia kwenye baraza la wafanyakazi umezingatia sifa zao kwenye utendaji pamoja na uwajibikaji ndani ya taasisi.

Pia, aliupongeza uongozi wa Wakala wa Vipimo unavyoongoza taasisi hiyo na kwa uongozi mahiri wa Mtendaji Mkuu pamoja na Jumuiya ya Wafanyakazi kwa ujumla na kwa kuona umuhimu wake kushiriki katika ufunguzi wa baraza jipya la wafanyakazi.

Alisema maendeleo ya taasisi ya WMA yanaonekana katika kutekeleza majukumu yake ya msingi ya kisheria ikiwa na jukumu kuu la kumlinda mlaji kupitia matumizi sahihi ya vipimo.

Alisema hayo ni mafanikio yanayonekana wazi hasa katika siku za karibuni wakati wakala imeanza kutoa huduma mpya za kuhakiki dira za maji na mita za umeme maeneo ambayo yalikuwa yakilalamikiwa kwa kiasi kikubwa na wananchi kwa kulipa gharama kubwa kuliko kiasi cha huduma wanayopata.

Aidha, Dk. Hashil aliwahamasisha wajumbe wa Baraza la Wafanyakazi kuunganisha nguvu zao kwa kufanya kazi kwa bidii, juhudi na maarifa ili kwa vitendo kuunga mkono juhudi za serikali kwa kutoa huduma bora na kupunguza kero na malalamiko ya wananchi dhidi ya serikali.

Aliwataka wajumbe wapya wa baraza kutumia nafasi vizuri kufanya tathmini ya kina ya jinsi walivyotekeleza majukumu yao ya kibajeti na kiufanisi katika mwaka uliopita na namna wanavyoweza kujipanga katika vipaumbele vya taasisi kwa mwaka ujao wa fedha ili kutimiza malengo ya serikali.

Alimshukuru Rais Dk. Samia Suluhu Hassan kwa maelekezo na miongozo yake ambayo inaisaidia wizara na taasisi zake kutekeleza mipango na mikakati ya kukuza uwekezaji, ufanyaji biashara na uendelezaji wa viwanda.



Katibu Mkuu wa ACT-Wazalendo, Ado Shaibu, akihutubia wananchi katika viwanja vya Baraza la Idd wilayani Tunduru ikiwa ni mwendelezo wa ziara ya chama hicho mikoani. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Vifo vitokanavyo na uzazi vyashtua

**Na Ashton Balaigwa,** MOROGORO

HOSPITALI ya Rufani Mkoa wa Morogoro imewaagiza wataalamu wa afya katika vituo vya afya kuongeza kasi ya kutoa elimu kwa wananchi kuhusu umuhimu wa kuwafikisha wagonjwa kwa wakati ili waweze kupata matibabu mapema kwa madaktari bingwa wakiwamo wajawazito.

Agizo hilo limekuja kutokana na kujitokeza kwa changamoto ya kimkoa kuhusu vifo vya wajawazito baada ya mwaka 2021/22 kuripotiwa jumla ya vifo 22 na mwaka huu kuanzia Januari hadi Machi kuwapo vifo 19.

Mganga Mfawidhi wa hospitali hiyo, Dk. Daniel Nkungu, alisema hayo wakati akiwasilisha taarifa ya uendeshaji na utoaji wa huduma kwa hospitali hiyo kwenye kikao cha Kamati ya Ushauri ya Mkoa (RCC), kilichofanyika Morogoro.

"Bado lipo tatizo la wagonjwa wengi wakiwamo wajawazito wanafikishwa hospitali ya rufani kutoka kwenye vituo vya afya wanakuja wakiwa tayari wamefikia hali mbaya na kuwasaidia inakuwa ni vigumu sana," alisema Dk. Nkungu.

Alifafanua kwa mwaka zaidi ya wanawake 5,000 wajawazito wanajifungua katika hospitali hiyo baada ya kupewa rufani na kati ya hao wanaojifungua kwa njia ya upasuaji ni zaidi ya 2,000 wakiwamo wanaopata huduma za kibingwa.

Alisema, kutokana na uwekezaji mkubwa uliofanywa na serikali ikiwamo mashine ya CT-SCAN, hospitali hiyo inatarajia kutoa mafunzo ya kutosha kwa watumishi wake ili kuongeza uwezo wao katika kutoa huduma bora kwa wananchi kwa kutumia vifaa vya kisasa.

Dk. Nkungu alisema hospitali hiyo pia imepata vifaa vya kuzalisha hewa tiba (oksijeni) na kabla ya hapo walikuwa wakinunua vifaa hewa tiba jijiji Dar es Salaam na Dodoma.

"Hivi sasa mtambo umesimikwa na kazi ya uzalishaji hewa tiba inaendelea na kwa sasa tutanunua kifaa cha kujazia hewa tiba kwenye mitungi ili kuwezesha hospitali zingine zinazohitaji ziweze kununua kutoka hospitali ya rufani ya mkoa," alisema Dk. Nkungu.

Naye Mganga Mkuu wa Mkoa wa Morogoro, Dk. Urio Kusirye, akifafanua suala la malipo kwa aina ya watoto wanaozaliwa katika hospitali hiyo kuwa changamoto hiyo imekuwa ikijitokeza kwa miaka miwili sasa.

"Wapo watu nimekutana nao wakinieleza hilo, lakini sisi tumeenda mbali zaidi kuhitaji risiti au kitu chochote chenye ushahidi wafike navyo kwetu ili kuthibitisha tuhuma hizo," alisema Dk. Kusirye.

Alisema hakuna gharama tofauti kati ya mtoto wa kike na wa kiume kulipishwa fedha wanapozaliwa katika hospitali hiyo.

Pia upo utaratibu wa msamaha wa malipo kwa wagonjwa ya kuruhusu mtu anayeshindwa kulipa asichangie huduma, cha msingi na anapopewa stakabadhi ya malipo humpasa kuwasilisha kwa utaratibu wa kupata msamaha ili kuweka mizania ya hesabu za makusanyo ya mapato.

**KABWELA** FADHILI MOHAMED



# Msajili wa vyama ailima barua TLP

**Na Sabato Kasika**

OFISI ya Msajili wa Vyama vya Siasa, imeuandikia barua uongozi wa Chama Tanzania Labour Party (TLP), ikiutaka kujieleze sababu za kuahirisha uchaguzi wa Mwenyekiti wa Taifa wa chama hicho.

Barua hiyo ya Machi 9, mwaka huu yenye Kumb: HA. 322/362A/38, iliyotiwa saini na Msajili Msaidizi wa Vyama vya Siasa, Sisty Nyahoza, inaelekezwa kwa Katibu Mkuu wa chama hicho, inataka hadi Jumatano ya wiki hii uongozi uwe umewasilisha maelezo katika ofisi hiyo.

Nyahoza anaeleza katika barua hiyo kuwa Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa ilipokea barua kutoka kwa baadhi ya wagombea wakilalamikia kuahirishwa kwa mkutano mkuu bila kufuata katiba na kanuni za chama hicho.

Barua hiyo inaendelea kueleza: "Kwa mujibu wa kifungu 5B cha Sheria ya Vyama vya Siasa Sura ya 258, uongozi wa TLP mnapaswa kuwasilisha maelezo kwa Msajili wa Vyama vya Siasa kujibu malalamiko ya wagombea hao."

Barua hiyo inaeleza kuwa majibu ya uongozi wa TLP yatasaidia kumfanya Msajili wa Vyama vya Siasa kujua ukweli kuhusu sakata hilo.

Mmoja wa wagombea wa nafasi ya Mwenyekiti Taifa, Mhandisi Aivan Maganza, alisema yeye na wenzake watatu ndio walioandika barua hiyo.

"Nilishirikiana na wenzangu akina Abdul Shangawe, Stanley Ndamugoba na Kinanzaro Mwanga baada ya kuona kumefanyika uhuni," alisema Mhandisi Maganza.

Katibu Mkuu wa TLP, Richard Lyimo, ambaye alikuwa mgombea wa nafasi hiyo, akithibitisha kupokea barua hiyo.

"Nimepokea barua hiyo na nitajibu kama nilivyoelekezwa na ofisi hiyo," alisema Lyimo.

Chama cha TLP kilitangaza uchaguzi huo ungefanyika Machi 6, mwaka huu, wajumbe 142 kutoka mikoa walihudhuria na wakiwa ukumbini walitangaziwa umeahirishwa hali iliyozua tafrani.

Uchaguzi huo unafanyika kutokana na kifo cha aliyekuwa Mwenyekiti wa TLP Taifa, Augustine Mrema, Agosti mwaka jana, huku nafasi hiyo ikikaimiwa na

na Hamad Mkadam aliyechaguliwa na sekretarieti ya chama hicho Septemba, mwaka jana.




Meneja Mawasiliano na Uhusiano wa Tanzania Commercial Bank (TCB), Gloria Mutta, akikabidhi misaada wa vitu mbalimbali kwa Ofisa Ustawi wa Jamii wa Hospitali ya Ocean Road Cancer Institute (ORCI), Devotha Kibanga, kwa ajili ya kusaidia wagonjwa wanawake wanaopatiwa matibabu katika hospitali hiyo, jijini Dar es Salaam ikiwa ni kusherehekea Siku ya Wanawake inayofanyika mwishoni mwa wiki. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Madaktari bingwa wa saratani ya ini kukutana Dar es Salaam

**Na Joseph Mwendapole**

MADAKTARI bingwa wa saratani ya ini nchini na wa mataifa mbalimbali duniani wanatarajiwa kukutana jijini Dar es Salaam wiki hii, kujadili namna ya kuboresha matibabu ya ugonjwa huo.

Mkutano huo ulioandaliwa na kikundi cha madaktari bingwa 'Liver Tumor Group', unaotarajiwa kufanyika tarehe 17- 18 wiki hii jijini hapo na utafunguliwa na Mganga Mkuu wa Serikali, Prof. Tumaini Nagu.

Kikundi hicho kinajumuisha madaktari bingwa wa upasuaji, mfumo wa chakula na ini, wataalamu wa tiba kwa njia ya radiolojia, tiba ya saratani kwa kutumia dawa na wa vipimo vya saratani (Pathologist).

Akizungumza na Nipashe juzi, daktari bingwa mbobezi wa upasuaji magonjwa ya mfumo wa chakula na ini wa Hospitali ya Taifa ya Muhimbili (MNH), Swalehe Pazi alisema mkutano huo ni wa kwanza kufanyika nchini.

Alisema kutakuwa na madaktari bingwa wa nchini na wengine bingwa kutoka mataifa ya Misri, Marekani, India, Malawi na Kenya na mada zitakuwa ni namna ya kukabiliana na ugonjwa huo kwa teknolojia ya kisasa.

Alisema takwimu za wagonjwa wa ini ni ngumu kupatikana kutokana na wengi kufia nyumbani na wengine hawafiki kupata huduma katika vituo rasmi. "Sisi wataalamu wa magonjwa ya ini tumedhamiria kutengeneza mfumo mzuri wa kuweka takwimu sahihi na za kisasa ambazo zitaisaidia serikali," alisema Dk. Mwanga.

Alisema kidunia kwa mujibu wa Shirika la Afya Duniani (WHO), inakadiriwa kuwa watu 500,000,000 duniani wanakufa kila mwaka kutokana na tatizo la ini na kwa mujibu wa shirika hilo, Tanzania inapata wagonjwa wengi.

"Kwa Tanzania bado hatuna takwimu sahihi kuhusu watu wanaokufa au kuugua magonjwa ya ini kwa sababu hatujawa na mfumo mzuri sana wa kukusanya takwimu hizi ndiyo sababu wataalamu wa Liver Tumor Group tunaandaa mfumo huo," alisema.

Dk. Mwanga, alisema kukosekana kwa takwimu za wagonjwa wa saratani ya ini ndiko kuliwasukuma madaktari bingwa kuanzisha kikundi cha Liver Tumor Group.

"Tuliona wagonjwa wanakuja wakiwa katika hali mbaya sana hapa Muhimbili na hatuwezi kusema liko kwa kiasi gani hapa nchini na matibabu yake yakoje kwa hapa nchini na kitu kingine kilichowasukuma madaktari kuanzisha kikundi hiki ni kutaka kujua je, ugonjwa huu hapa nchini unafanana na duniani kote? Na je, tiba inayotumika huko nje inaweza kutumika kutibu hapa nchini?" Alisema.

Aidha, alisema kwa kawaida ugonjwa huo huwapata watu wazima kuanzia miaka 60, 70 na kuendelea kwenye mataifa mengi duniani, lakini kwa Tanzania unawapata hata vijana wenye miaka 15, 20 hali ambayo imewafanya wataalamu wajiulize huenda ugonjwa ni tofauti na matibabu ni tofauti.

"Hivyo tukaona kuna haja ya kuungana kujua ukubwa wa tatizo hili hapa nchini na kufanya tafiti kujua je, ugonjwa huu unaozungumzwa duniani ni huo huo unaowapata Watanzania na kushirikiana na wenzetu duniani kukabiliana na tatizo hili," alisema Dk. Mwanga.

Alisema wameanzisha utaratibu wa kila Ijumaa madaktari wataalamu wa magonjwa ya ini kwa pamoja wakimuona kila mgonjwa wa ini aliyepatiwa matibabu MNH.

Kuhusu ukusanyaji wa takwimu za wagonjwa wa ini, Dk. Mwanga alisema wameanzisha mfumo wa kuwasajili wagonjwa wote nchini unaoitwa, Liver Cancer Registry, mgonjwa yeyote atakayetibiwa saratani ya ini atasajiliwa.

"Kuanzia hapo tutakuwa na uwezo wa kusema kwa mwaka huu wagonjwa waliotibiwa saratani ya ini ni kiwango fulani kwa hiyo tutaweza kujua tatizo liko kwa ukubwa gani kwa hiyo mkutano huu unalenga kutoa elimu kwa umma kuhusu ugonjwa huu," alisema.

Alisema kupitia kikundi hicho watatoa elimu ili kila mwananchi afahamu dalili za ugonjwa huo na afahamu anakotakiwa kumpeleka mgonjwa wa saratani ya ini kwa ajili ya kupatiwa matibabu sahihi kuokoa maisha yake.

# Wanawake wahimizwa kutumia fursa biashara utalii

**Na Mwandishi Wetu**

TAASISI isiyo ya kiserikali ya 'Fungua Trust' imehimiza ushiriki wa wanawake katika biashara za utalii.

Mbunge wa Bunge la Afrika Mashariki anayeiwakilisha Tanzania na Ofisa Mtendaji Mkuu wa Fungua Trust, Dk. Shogo Sedoyeka, alitoa rais hiyo alipokuwa akizungumza katika kongamano la kuadhimisha Siku ya Wanawake Duniani lililofanyika Machi 7, mwaka huu.

Alisema ujumbe wa mwaka huu wa Siku ya Wanawake Duniani ni ubunifu na mabadiliko ya teknolojia katika kuleta chachu kwa usawa wa kijinsia na mawasilisho yaliongozwa na ujumbe: 'Teknolojia-bunifu kwa wanawake katika sekta za utalii'.

Alisema sababu ya kujikita kwenye sekta ya utalii ni kutokana na kutoa fursa nyingi za kuongeza kipato kwa wanawake, vijana na wenye ujuzi au mtaji mdogo.

Aliongeza kuwa ingawa fursa hizo zinaonekana kuwa nyingi kwa makundi yote katika jamii, uwezo mdogo kiteknolojia na kiubunifu ni moja ya changamoto zinazowarudisha nyuma wanawake wengi kushiriki kikamilifu katika biashara ndani ya mnyororo wa utalii.

Alisema kuwa taasisi hiyo ilianzishwa kwa lengo la kuongeza uwezo wa jamii zilizo katika mazingira magumu nchini Tanzania na ndani ya ukanda wa Afrika Mashariki, kutumia fursa zilizopo kuleta mabadiliko chanya katika maisha.

Naye Balozi Fatuma Ndangiza, Mbunge wa EALA kutoka Rwanda ambaye ni Katibu Mkuu wa Umoja wa Wanawake Bunge la Afrika Mashariki, alibainisha kuwa kaulimbiu ya mwaka huu inatambua nafasi ya teknolojia na ubunifu katika kukuza usawa wa kijinsia na kuwataka wadau wa EAC kuchukua hatua ili kuharakisha ujumuishaji wa kidijitali na mikakati ya usawa bila kuacha mtu nyuma.

Alisema ubunifu na teknolojia ndiyo vichocheo muhimu katika kuharakisha ukuaji wa utalii, ushirikiano wa kikanda, kufikia ajenda ya AU 2063 na malengo ya Maendeleo Endelevu ya Umoja wa Mataifa.

Ili kuleta uwiano wa kidijitali na kupunguza vikwazo vya kijinsia katika teknolojia kwa wanawake kwenye biashara za utalii Ndagiza alishauri kuweka kipaumbele kwenye uwekezaji wa utalii na teknolojia jumuishi; kukuza ushiriki wa wanawake katika sayansi, teknolojia na TEHAMA; na utetezi wa sera na mifumo ya kisheria kuongeza usalama kwa wanawake na wasichana.

Majadiliano ya wadau yalisisitiza umuhimu wa kuwa na vyanzo vya kimkakati vya mitaji itakayowezesha wanawake kuanzisha na kukuza biashara za utalii pamoja na kuongeza uwezo wa wanawake kutumia ubunifu wa kiteknolojia kwa kupitia mafunzo.

Kwa upande mwingine serikali ilihimizwa kuweka kipaumbele katika uibuaji wa mazao mapya ya utalii mathalan utalii wa matibabu (medical tourism).

Ili kufanikisha hili serikali imeombwa kuweka miongozo mahsusi kupitia kanuni za usimamizi, kupitisha sera zitakazoinua zao hili, pamoja na kuongeza msaada wa kiufundi kwa wadau wa sekta.



# Madiwani waunda kamati ya kuchunguza uharibifu mazingira

**Na Godfrey Mushi,** HAI

MADIWANI wa Halmashauri ya Wilaya ya Hai mkoani Kilimanjaro wameunda kamati ndogo kuchunguza uharibifu wa mazingira katika chemichemi za Shiri na Kimamiri baada ya kuvamiwa na wananchi wanaoendesha shughuli za kilimo.

Maeneo mengine yanayotishiwa na jangwa ni Mto Kikafu na Mto Weruweru, ambayo baadhi ya wafanyabiashara na baadhi ya wananchi wanadaiwa kuendesha operesheni ya siri ya ukataji miti ovyo kwenye kingo za mito hiyo.

Akiwasilisha hoja ya dharura katika Baraza la Madiwani la Halmashauri hiyo juzi, kuhusu tishio hilo la uharibifu wa mazingira, Diwani wa Kata ya Mnadani, Nasibu Mndeme, alisema hali ni mbaya katika vyanzo hivyo vya maji kutokana na kukithiri kwa kilimo cha mboga aina ya saladi katika chemichemi ya Shiri.

Mndeme, ambaye ni Mwenyekiti wa Kamati ya Elimu, Afya na Maji, alisema: "Ukiangalia kwenye kingo za mito, mabonde pamoja na vyanzo vya maji, kwa mfano chemichemi ya shiri, kumeotesha katikati ya chemichemi mboga aina ya saladi na chemichemi ya Kinamiri zimeathiriwa na hazina maji.

"Lakini mbaya zaidi, wanatumia sumu kwa ajili ya kupulizia mboga zisishambuliwe na wadudu na wakati maji hayo yanatumika kwa shughuli za umwagiliaji na matumizi mengine.

"Kwenye kingo za mito yetu, wako wanaovitumia kutengeneza pombe haramu ya gongo na mabaki yake wanayamwaga kwenye maji na mabaki hayo yanakwenda kuharibu mazao ya wananchi.

Zaidi aliongeza: "Ukataji miti ovyo katika vyanzo vya maji ambao umekithiri sana na ukijaribu kuangalia kwenye maeneo mbalimbali ndani ya wilaya yetu baadhi yameathirika na suala hili."

Akitangaza uamuzi wa baraza kuhusu hoja hiyo, Mwenyekiti wa Halmashauri hiyo, Edmund Rutaraka, alisema ameamua kuunda kamati ndogo ya kuchunguza sakata hilo na ameipa muda wa mwezi mmoja kuwasilisha ripoti.

Alisema: "Nimeunda kamati ndogo kufuatilia suala hili na itaongozwa na Mwenyekiti wake ambaye ni mtoa hoja (Mndeme), Mashoya Natai (Diwani wa Masama Magharibi), Hausen Nkya (Diwani wa Viti Maalum) na Upendo Sawe (Diwani wa Viti Maalum).

Aliongeza: "Natoa muda wa mwezi mmoja kwa sababu najua kuna vikao vutaendelea hapa na Mkurugenzi uweke watu wako kama ni wawili, watatu ili wakafanye kazi hiyo na tuweze kupata taarifa rasmi".



Mbunge mstaafu wa Jimbo la Muheza mkoani Tanga, Hebert Mntangi, akinyoosha mikono ya furaha juzi baada ya kumaliza kuzungumza katika mkutano wa Halmashauri Kuu ya CCM Wilaya uliofanyika mwishoni mwa wiki. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

## Wanawake TRA watoa msaada kituo cha watoto yatima

**Na Jaliwason Jasson,** BABATI

MAMLAKA ya Mapato Tanzania (TRA), imepeleka misaada ya kibinadamu kwenye kituo cha kulelea watoto cha MaHOCE kilichoko Wilaya ya Babati.

Ofisa Mwandamizi wa TRA, Mkoa wa Manyara, Amina Muhombe, akizungumza na Nipashe jana baada ya kukabidhi misaada ya kibinadamu alisema wametoa msaada huo kama sehemu ya maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani.

Alisema idadi ya watoto wanaofanyiwa ukatili inaongezeka kutokana na wanawake wengi kujihusisha na vitendo hivyo ama kwa watoto wao wa kuzaa au kurithi.

Aidha, alisema watoto hao katika vituo wanaongezeka kutokana na kutelekezwa.

"Tuwatumie ustawi wa jamii na mamlaka nyingine zinazohusika ili tuweze kumaliza matatizo yetu na siyo kutupa watoto," alisisitiza.

Kuhusu misaada ya kibinadamu, Ofisa Mwandamizi wa TRA mkoani humo, Zuwena Abdalla, alivitaja vitu ambavyo wamekabidhi kwa kituo hicho kuwa ni maharage kilogramu 25, sabuni ya unga mifuko mitatu na unga wa ngano mifuko mitatu ya kilogramu 25.

Vingine ni mafuta ya kula ndoo tatu, madaftari dazeni moja na sabuni ya kipande katoni mbili.

Mwakilishi wa MaHOCE, Anderson Mbwambo, aliwashukuru wafanyakazi hao wanawake wa TRA kwa kuwapa msaada huo, huku akieleza kikwazo wanachokutana nacho ni bidhaa mbalimbali kama chakula kupanda bei tofauti na bei za awali wanazokuwa wamepanga.

# Tisa wakutwa na tishio la saratani ya mlango wa kizazi

**Na Woinde Shizza,** ARUSHA

KAMBI maalum ya uchunguzi na matibabu ya saratani iliyofanyika jijini Arusha, chini ya madaktari bingwa wa saratani kutoka Taasisi ya Saratani Ocean Road (ORCI), imegundua wagonjwa tisa wanaotishiwa na saratani za mlango wa kizazi.

Wanawake wanne kati yao wamebainika kuwa na viashiria vya mabadiliko ya awali ya saratani ya mlango wa kizazi na watano wamekutwa wana viashiria vya kuwa na saratani ya mlango wa kizazi.

Kwa mujibu wa ripoti iliyotolewa na Meneja Huduma ya Kinga ya Saratani kutoka taasisi hiyo, Dk. Maguha Stephano, wanawake wanne wenye viashiria vya mabadiliko ya awali wamepatiwa tiba ya kukinga.


Aidha, wanawake watano waliokutwa na viashiria vya kuwa wa na saratani ya mlango wa kizazi wamechukua sampuli ya vinyama kwenye mlango wa kizazi kwa ajili ya kuvifanyia uchunguzi zaidi.

"Tumekuja na madaktari bingwa wa uchunguzi wa sampuli za vinyama au majimaji/damu mwilini ili kuangalia uwepo wa chembe chembe za saratani.

"Kwa hiyo pia, majibu watayapata muda mfupi ujao na wakithibitika kweli wana tatizo hilo tutawapeleka Ocean Road, kwa ajili ya matibabu,"alisema Dk. Maguha.

Katika ripoti yake, Dk. Maguha, ameeleza kuwa ugonjwa wa saratani nchini unaonekana kuwa tatizo linaloongezeka kila mwaka, hususani saratani ya mlango wa kizazi.

Alisema kati ya wagonjwa 100 wenye saratani za aina mbalimbali, wagonjwa 47 wanakutwa na saratani ya mlango wa kizazi.





# SHIRECU kufufua viwanda vya kuchakata mazao

**Na Marco Maduhu,**
SHINYANGA

CHAMA Kikuu cha Ushirika mkoani Shinyanga (SHIRECU), kimeweka mikakati ya kufufua viwanda vya kuchakata mazao, ili kuimarisha ushirika pamoja na kumkomboa mkulima kiuchumi.

Kwa mujibu wa Mwenyekiti wa chama hicho, Kwiyolecha Nkilijiwa, katika mwaka huu wamejiwekea malengo mbalimbali ya kujiimarisha ikiwamo na kufufua viwanda vya kuchakata mazao ili kumkomboa mkulima pamoja na kuongeza vyanzo vya mapato na kupunguza madeni ya mikopo ambayo wanadaiwa.

Akieleza juu ya suala la ufufuaji wa vyama hivyo, Mbunge wa Kishapu, Boniphace Butondo, alisema vyama vikuu vya ushirika vinapaswa kufufuliwa na kushikwa mkono na serikali pamoja na kupewa mitaji ili vianze kununua mazao na kuchakata na kujiendesha kwa faida pamoja na kumwinua mkulima.

Mbunge wa Viti Maalumu mkoani Shinyanga, Christina Mzava, alisema upo umuhimu wa kuirejesha SHIRECU mpya ili iendelee kuwa mkombozi kwa mkulima, huku akiwataka mikopo ambayo wamekuwa wakikopa itekeleze malengo yaliyokusudiwa pamoja na kuacha kuzalisha madeni ambayo hayana tija.

Aidha, aliviomba vyama vya msingi vya ushirika viache tabia ya kukopa wakulima pale wanapokuwa wakiuza mazao, bali walipwe fedha zao kwa wakati ili kumhakikishia maisha bora mkulima.

Mkuu wa Wilaya ya Shinyanga, Johari Samizi, alivitaka vyama vya ushirika kutekeleze majukumu yao ipasavyo kwa kujiimarisha pamoja na kuinua uchumi wa mwananchi kupitia ununuzi wa mazao kwa bei rafiki.

Alisema hali hiyo itawasaidia kuendelea kuaminika na kumfanya mkulima aendelee kuona faida ya kilimo katika maisha yake na umuhimu wa vyama vya ushirika katika kuboresha maisha yao.



Wajumbe wa Mkutano Mkuu wa Chama Kikuu cha Ushirika mkoani Shinyanga (SHIRECU), wakiwa kwenye mkutano kujadili mambo mbalimbali kwa ajili ya kuimarisha ushirika huo ikiwamo kufufua viwanda vya kuchakata mazao (Ginery) ili kumkomboa mkulima kiuchumi kwa kununua mazao yake kwa bei rafiki. **PICHA: MARCO MADUHU**

## Viongozi h'shauri wakumbushwa wajibu wao kazini

**Na Titus Mwombeki,**
KAGERA

VIONGOZI wa Manispaa ya Bukoba wametakiwa kuongeza weledi kazini na kuhakikisha wanatimiza wajibu wao katika kuwahudumia wananchi na kujiepusha na baadhi ya watu wenye nia ya kutaka kuwagombanisha katika utendaji kazi wao.

Kauli hiyo imetolewa mwishoni mwa wiki na Mbunge wa Bukoba Mjini, Steven Byabato ambaye ni Naibu Waziri wa Nishati, wakati akihutubia wananchi katika mkutano.

Byabato aliwataka viongozi kutoka ngazi zote katika Manispaa ya Bukoba kuzingatia majukumu yao katika kumuhudumia mwananchi.

Byabato alisisitiza kuwa wapo watu wenye nia ovu wanaokuja kwake na wengine wanakwenda kwa viongozi wakiwa na lengo la kuwachonganisha, suala ambalo linakwamisha maendeleo Bukoba.

"Fanyeni kazi kupitia maadili yenu ya kazi, Bukoba itajengwa na wana Bukoba wenyewe, tukigombana hatutafika mbali achana na watu wanapiga fitina na kuchonganishana sisi tumeapa kama viongozi wa serikali pamoja na chama hatutagombana, tumejipanga kuleta maendeleo Bukoba," alisema.

Mstahiki Meya wa Manispaa ya Bukoba, Gybson Godson, aliwaomba wananchi wa manispaa hiyo kuendelea kuwaamini viongozi wao kwani wamejizatiti kuiletea maendeleo Bukoba.

Katibu Mwenezi wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Mkoa wa Kagera, Amimu Mohamud, aliwata viongozi waliochaguliwa kuendelea kuchapa kazi kwa bidii na kuinadi ilani ya CCM kama inavyowaelekeza.

## Waziri Mkuu mgeni rasmi wiki ya nenda kwa usalama kitaifa

**Na Rose Jacob,** MWANZA

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, leo anatarajiwa kuongoza Watanzania katika maadhimisho ya wiki ya nenda kwa usalama ambayo kitaifa yanafanyikia mkoani Mwanza.

Maadhimisho hayo yanatarajiwa kuudhuriwa na viongozi mbalimbali wa serikali pamoja vyombo vya usalama barabarani, yatafanyika katika viwanja vya Furahisha mkoani hapo.

Hayo yalisemwa jana na Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, Adam Malima na kueleza kuwa lengo kuu la maadhimisho hayo ni kutoa elimu ya sheria, kanuni na taratibu za usalama barabani kwa makundi yote ya watumiaji wa barabara.

Alisema katika kipindi cha Januari hadi Desemba 2020, zimeripotiwa ajali kubwa 81 zilitokea Mwanza zilizosababisha vifo vya watu 71, majeruhi 96.

"Kwa upande wa pikipiki zimetokea ajali 30 na kusababisha vifo vya watu 25 majeruhi 26 mwelekeo wa takwimu hizo siyo nzuri, nawataka watumiaji wa barabarani na wamiliki wa vyombo vya moto kufuata sheria na kanuni, kuepuka mambo yanayosababisha ajali," alisema Malima.

Aidha, alitaja sababu za kutokea kwa ajali kuwa ni pamoja na mwendokasi, ubovu wa vyombo vya moto, ulevi, uendeshaji wa kutochukua tahadhari, kujaza abiria na mizigo uliopitiliza na kuegesha magari mabovu yaliyoharibika barabarani kwa muda mrefu.

Malima alisema kutokana na ajali hizo Mkoa wa Mwanza umeandaa sheria ndogo ya matumizi ya barabara ili kukomesha ajali za mara kwa mara.

Kamanda wa Kikosi cha Usalama Barabarani, Kamishna

Msaidizi Mwandamizi wa Polisi, Ramadhan Ng'azi, aliwataka wamiliki wa vyombo vya moto, kufika polisi kwa ajili ya ukaguzi na kupewa elimu ya usalama barabarani.

Alisema; "Nawasihi abiria kutoshabikia vitendo vya ukiukwaji wa sheria husasani mwendokasi, mnatakiwa kukemea na kutoa taarifa kwa Jeshi la Polisi wakati mnapoona viashiria vya usababishaji wa ajali unaofanywa na madereva."

Nipashe
# TESA
Jumanne Machi 14, 2023
TEKNOLOJIA • ELIMU • SAYANSI



Ukurasa 12
Hamasa, umuhimu chanjo ya kuzuia saratani shingo ya kizazi kwa mabinti



Ukurasa 14
Ushoga na ndoa za jinsi moja unavyopingana na maumbile



Ukurasa 13
**MIAKA 2 RAIS SAMIA Anavyowatoa gizani 1,600 waliokwama kusoma ni wa sekondari, takwimu za msingi zaandaliwa**

ELIMU

NA CHRISTINA MWAKANGALE

# Mabinti sikilizeni somo la aliyenusurika ndoa utotoni

## •Anawakumbusha semeni 'no' kwenye kuonewa

"NAFANYA hii kazi kwa sababu na mimi niliwahi kupitia shida kama hii, nimekutana na mambo makubwa tena wakati nikiwa mdogo mwenye miaka 14 nilinusurika kuozwa tena na ndugu zangu wala si wazazi wangu. Nilikataa." Ni ushuhuda wa Debora Timothy.

Anakizungumza na Nipashe, hivi karibuni jijini Dar es Salaam, wakati wa maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani, anaeleza wazi na kutaka kuacha somo kwenye jamii kwamba mtoto wa kike anahitaji kulindwa na familia, jamii na taifa.

Akieleza yaliyomfika kwa ujasiri anatoa hadithi ya maisha yake hatua kwa hatua, akisema maisha yake yanajaa juhudi za kuhamasisha mabadiliko na kwamba ni 'young reporter', mtoa taarifa na mwanaharakati kutoka Mwanza, akifanya kazi na Shirika la Kiota Women's Health and Development (KIWOHEDE).

Debora Timothy, aliyezaliwa mwaka 2000 mkoani Mwanza, miaka saba baadaye mama yake mzazi alifariki dunia. Malezi yake yakahamishiwa kwa bibi mzaa baba yake, ingawa hadi anafikia umri huo, hakuwahi kumfahamu baba yake.

"Nimelelewa na bibi peke yake, simjui baba yangu, nakumbuka siku moja nilisikia ndugu zake wakipiga simu, wakimwambia wewe mke wako kafariki, unakuja lini. Sikujua alichowajibu, ila nilikuwa nawaona ndugu zake baba mdogo na wengine wakija kwa bibi," anasema Debora.



Shujaa wa kupinga ndoa za utotoni na ukatili kwa wanawake na watoto, Debora Timothy.**PICHA CHRISTINA MWAKANGALE.**

Alianza shule, ingawa baada ya miaka michache, bibi yake aliyekuwa anamlea alifariki dunia akisimulia kuwa alipenda kusali na kila alipokwenda kanisani kwa siku za ibada na nyinginezo aliongozana naye.

"Nafikiri kadri siku zilivyokuwa zinakwenda aliibaini siku zake za kuishi zinapungua, alikuwa anamwomba mchungaji wake kuwa iwapo atakufa anichukue, anilee," anakumbuka Debora.

Anakumbuka kuwa tangu bibi alipowasilisha ombi hilo kwa mchungaji haukupita mwezi akafariki. Hata hili jina la Timothy, si la baba yake ni la mchungaji, ambaye alichukua majukumu ya baba mlezi, kumsomesha hadi hapa alipo akikaribia miaka 23.

Debora anasema baada ya bibi yake kufariki, kikao cha ndugu kikakaa: "Kilipofanyika kikaamua kila mtu achukue familia yake nikachukuliwa na baba mdogo, nikawa nazunguka kwa jamaa zangu, nakaa miezi michache kwa kila ndugu.

Anasimulia kuwa baba yake mkubwa alimpokea, moyoni akajua huyu atakuwa mtu sahihi lakini naye baada ya mwezi akamtafutia kazi za ndani licha ya kwamba wakati huo ni mdogo bado lakini pesa za mshahara alizokuwa analipwa akawa anazichukua.

"Akaja mwajiri wangu nilipokuwa nafanyakazi kwake, akasema jiandae unarudi kwenu, akanipa hela na nauli nafika tu kwa dada akaniambia nina habari njema kwako kuwa unaolewa, licha ya kwamba nilikuwa na miaka 14. Na huyo mchumba niliambiwa alikuwa ni mtu mzima. Nikamwambia siwezi kabisa kufanya hivi, wakanishauri lakini nikakataa kuolewa."

Anaongeza kuwa baba mkubwa alimwadhibu na usiku huo aliondoka na kutembea usiku kucha hadi akampata mchungaji akamtetea na ndugu wakawa hawamtaki tena kumsikia.

"Mchungaji akanichukua na kunilea mpaka sasa na nikawa nawaza nitapata wapi muda na mimi nije nitoe au nipaze sauti kwa mabinti wenzangu, ili wasaidiwe, nikawa napata semina nafundisha kitu kilichonipata nikiwa na ukweli ndani ya moyo kwa sababu nimepitia changamoto hiyo."

Aidha, anasema tangu darasa la tatu anaishi kwa mchungaji na alipomaliza la saba, alianza masomo ya QT hadi kidato cha nne na kushiriki mafunzo ya kompyuta na sasa anafanya kazi kwenye kituo cha kulea watoto 'day care' iliyoanzishwa na mchungaji.

**ALIPO LEO**

Debora anasema mradi wa kupinga ukatili wa kijinsia ulianza mwaka 2009 ukiwa na mabinti 30 wakifanya kazi kwenye kata nne na kwamba wanatoa elimu kwenye shule, zahanati majumbani na sehemu zenye mikusanyiko ya watu mbalimbali kwenye kata za Buzuruga, Kisesa, Buhongwa na Mhandu.

"Mradi huu unapambana kutokomeza rushwa ya ngono na kimtandao Mwanza pia tunatoa elimu na kufanya kazi kwa vitengo mfano kwa kata ya Buzuruga wanafanya siku yao na kata zingine pia vivyo hivyo," anasema Debora.

"Kikubwa kazi ifanyike kwa wakati, tuna vitu vingi ambavyo tunavipeleka katika jamii na kupambana navyo usiku na mchana hususani kwa wale waandishi wadogo mmoja wapo ni mimi na hapo wapo mabingwa na sisi wadogo."

**CHANGAMOTO**

Ukatili kwa watoto hasa kubakwa ni changamoto anazozitaja, akitoa mfano dereva wa bodaboda katika kata mojawapo alimnajisi mtoto aliyekuwa akienda shuleni mwenye miaka 10.

Anaeleza kuwa dereva huyo alimwambia binti mwanafunzi huyo anampeleka shuleni lakini alikataa lakini bodaboda akatumia mbinu nyingi, akamwambia kitu

INAENDELEA UK.12

ELIMU

NA WAANDISHI WETU

# Hamasa, umuhimu chanjo ya kuzuia saratani shingo ya kizazi kwa mabinti



Mabinti wakipatiwa chanjo ya kuzuia saratani ya shingo ya kizazi wanaweza kuepuka magonjwa hayo siku zijazo. **PICHA: MTANDAO**

Ni Wiki ya Kinamama Duniani baada ya kuadhimisha siku maalumu ya wanawake iliyofikia kilele Machi 8, wakati huu shamra shamra zikiendelea kumekuwapo na mijadala kuhusu mienendo na hali za wazazi hasa kinamama wa sasa.

Ni kutokana na mabadiliko na hali zao kuwa tofauti na vile jamiii ilivyozoea kuwaona wazazi kama hao miaka ya nyuma. Hata hivyo zaidi kumekuwa na wimbi kubwa la magonjwa ambayo yanawakabili kinamama hivyo kusababisha kundi hili kuwa na matatizo ya kiafya ambayo pia huathiri jamii hasa watoto na wategemezi wengine.

Baadhi ya magonjwa hayo ni saratani ya mlango wa kizazi, ya matiti, kuota nyama au 'faibroid' kwenye mfuko wa uzazi kuwa na vitambi na uzito uliopitiliza pia yapo matatizo mengi yanayoibuka wakati wa uzazi, kifafa, kisukari vyote vinavyoambatana na uzazi vikitajwa.

Hata hivyo, lengo kuu la makala hii ni kuangalia jinsi jamii inavyowaandaa kinamama bora wa baadaye kwa kuwapa elimu, chanjo na huduma nyingine za kiafya dhidi ya saratani ya mlango wa kizazi ambayo zama hizi ni kitisho.

Tanzania inawaandaa wazazi wa kesho kwa kuwaepusha na maradhi hasa ya saratani ya mlango wa uzazi. Kansa hiyo ya mlango wa kizazi inaweza kusababishwa na virusi vya Human Papilomar Virus (HPV), ambavyo pia husababisha nyinginezo kama ya ukeni, uume, kwenye njia ya haja kubwa hata kwenye koo inayoitwa saratani ya 'oropharyngeal'.

**MAONI KITAALAMU**

Kadiri ya tafiti zilizofanywa kuhusu tatizo la saratani ya mlango wa kizazi maeneo mbalimbali duniani, zinaonyesha kuwa ugonjwa huu huwapata wanawake hasa wale ambao hawakupata chanjo HVP ambayo hupewa watoto wa kike wa umri wa kati ya miaka 9 na 14. Kinga hiyo, hutolewa katika maeneo ndani ya jamii hasa shuleni na pale ambapo wanaweza kufikiwa kwa urahisi.

Mwaka 2014 Tanzania ilizindua utoaji wa chanjo hiyo ili kuwanusuru wasichana na uwezekano wa kupata kansa ya shingo ya kizazi.

Aidha, chanjo hiyo imethibitika kuzuia saratani ya mlango wa kizazi kwa karibia asilimia 90. Hivyo wataalamu wanashauri watoto wa kike wa umri kati ya miaka tis ana 15 kupatiwa HVP ili kuwakinga na tatizo la saratani ya kizazi.

> “Baadhi ya magonjwa hayo ni saratani ya mlango wa kizazi, ya matiti, kuota nyama au 'faibroid' kwenye mfuko wa uzazi kuwa na vitambi na uzito uliopitiliza pia yapo matatizo mengi yanayoibuka wakati wa uzazi, kifafa, kisukari vyote vinavyoambatana na uzazi vikitajwa.

Serikali imeendelea na juhudi za kupambana na ugonjwa huo hatari katika jamii ikiwa ni pamoja na kutoa elimu na chanjo bila malipo kwa wananchi na mabinti katika maeneo mbalimbali. Moja ya wadau wakubwa wa kupambana na ugonjwa wa saratani ya mlango wa kizazi nchini ni Shirika la Marekani la kupambana na UKIMWI kwa watoto wadogo la EGPAF.

Elizabeth Glaser Pediatric Aids Foundation (EGPAF) Tanzania, inahudumia mikoa ya Kilimanjaro, Arusha, Manyara, Dodoma, Singida na Tabora, hivyo wananchi hasa wale wenye watoto wa kike wa umri wa miaka tisa mpaka miaka 14 wanahimizwa kuongea na mabinti wao kuhusu kuwapo kwa tatizo hilo na umuhimu wa kujitokeza kupata chanjo hiyo.

Japo upo mchango walimu shuleni wanaojitahidi kufanya jukumu hilo la kuongeza uelewa wa wanafunzi hasa wale wa kike juu ya umuhimu wa chanjo hii.

**UMUHIMU WA CHANJO**

Kama watoto wengi wa kike watapata elimu na chanjo dhidi ya ugonjwa wa saratani ya mlango wa kizazi, huenda jamii itapunguza kwa kiasi kikubwa ongezeko la ugonjwa kwa siku zijazo.

Hii itakuwa ni juhudi mojawapo ya kuwaandaa watoto wa kike wa sasa ili waweze kuja kuwa kinamama bora wa baadaye wasiokuwa na changamoto kubwa ya saratani ya mlango wa kizazi.

**USHAURI**

Wito kwa jamii ni kuwa kila mwanajamii ajitahidi kuwaandaa watoto wa kike ili waweze kuwa mama bora wa baadaye ikiwa ni pamoja na kuwapa elimu ya kuwasaidia kujikinga na ugonjwa wa saratani ya mlango wa kizazi.

Zaidi ya watoto wa kike walio kati ya miaka tisa na 14 ambao ni umri wa kupata chanjo ya kujikinga na saratani ya mlango wa kizazi wajitokeze kupata chanjo dhidi ya ugonjwa huo. Hii itawasaidia wao kuja kuwa mama na wazazi bora wa baadaye katika maisha yao na jamii inayowazunguka.

***Imeandaliwa na EGPAF, Pankras Luogai MUHAS, Dr. Safina Yuma wa Wizara ya Afya, Idara ya Afya ya Uzazi, Mama na Mtoto.***

# Mabinti sikilizeni somo la aliyenusurika ndoa

INATOKA UK.11

kilichomvuta mtoto akakubali, na huo ukawa mwanzo wa kunajisiwa kwa mtoto huyo mwenye miaka 10 mwanafunzi wa darasa la nne.

Baada ya kupakiwa kwenye pikipiki hakupelekwa shuleni ila kwenye jengo ambalo halijakamilika kamfanyia ukatili na kelele za binti huyo zikamshtua mpitanjia aliyekwenda moja kwa moja kuangalia ndani ya jumba na kumnasa bodaboda akitenda ukatili na kufanikisha kumkamata na kesi ikafikishwa kwao na kuna baadhi ya wanaharakati wanatoa elimu kuhusu ukatili.

Debora, anaeleza kuwa kesi imefika mahakamani lakini wakaanza kupigwa tarehe na changamoto ikawa baba mtoto hataki kesi ifike mbali na wakati huo, mama yeye anasema lazima haki ikitendeke na kwamba hofu yao baba amepokea kitu kidogo kutoka kwa mshtakiwa.

“Mama akahakikisha kesi inasonga mbele na sisi tukasimama upande wa mama na mashtaka yanasonga mbele ikaenda na kupangiwa tarehe na mtu wa kundi letu akafika mahakamani na baba akikazana kesi iishe na tukafika mbali, huku chini kabisa ushirikiano ukawa unapotea.”

Anatoa ushauri kwa wazazi akisema wakumbuke kuwapa fursa wasichana, kielimu na kuonyesha vipaji vyao, badala ya kufikiria ndoa ni muhimu katika umri mdogo ili wasichane wasiwe wahanga wa mimba za utotoni.

ELIMU

## NA SABATO KASIKA

MIAKA 2 RAIS SAMIA

# Anavyowatoa gizani 1,600 waliokwama kusoma ni wa sekondari, takwimu za msingi zaandaliwa

UPO msemo kuwa mbaazi zikikosa maua hulisingizia jua. Lakini kwenye awamu ya Rais Samia Suluhu Hassan, hasa inapotajwa sekta ya elimu mbaazi hazitakuwa na kisingizio kwanini 'hazikusoma.'

Ni juhudi za serikali za kugharamia elimu msingi sekondari na hata kuwarejesha shuleni wale walioanguka kutokana na matatizo mbalimbali iwe ujauzito, kukosa ada, maradhi na ugumu wa maisha ya familia. Hivyo itakuwa ngumu kueleza kwanini bado wewe ni mbumbumbu.

Rais Samia anapoelekea kufunga miaka miwili, tangu alipoapishwa kushika nafasi hiyo, Machi 19 mwaka 2021 baada ya kifo cha mtangulizi wake, Hayati Dk. John Magufuli.

Tangu wakati huo aliposhikia madaraka, yapo mengi ambayo serikali yake imeyafanya, katika sekta mbalimbali, kwa lengo la kutaka nchi inazidi kupiga hatua kwenda mbele kwenye maendeleo.

Miongoni mwa sekta hizo, ni ya elimu ambapo katika kipindi cha miaka miwili ya uongozi wake, amehakikisha wanafunzi waliokatisha masomo kutokana na sababu mbalimbali ikiwamo mimba, wanarudi shuleni kuendelea na masomo.

Hadi kufikia Januari mwaka huu tangu Rais alipotoa maelekezo mwaka juzi, wanafunzi 1,692 walikuwa wamerudi shuleni, kuendelea na masomo katika shule mbalimbali za sekondari ni kwa mujibu wa Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Omari Kipanga.

Anatoa ufafanuzi huo bungeni jijini Dodoma mwaka huu na kuongeza kuwa wizara inaendelea kukusanya takwimu za shule za msingi na huenda wanafunzi waliorejea madarasani wakawa wengi zaidi na hiyo ni kazi kubwa ya kuwainua wanawake na mabinti.



Rais Samia Suluhu Hassan.

Aidha, anasema ili kumaliza tatizo hilo la mimba shuleni, serikali imeweka mikakati minne ukiwamo wa Rais Samia kuridhia kujengwa shule 26 za sekondari za wasichana ambapo kila mkoa utakuwa na moja,

Kipanga anataja mkakati mwingine wa serikali kuwa ni kuanzisha vitengo vya elimu ya unasihi na ushauri, katika shule mbalimbali, ili kuhakikisha vitendo vya unyanyasaji visijitokeze.

"Pamoja na hiyo, mkakati mwingine wa serikali ni kuchukua hatua kwa wale wote wanaohusika, katika vitendo vya kunyanyasa wanafunzi, ili wachukuliwe hatua za kinidhamu," anasema Kipanga.

Wakati Rais akiendelea na juhudi za kukomboa mtoto wa kike kielimu, sakata la mimba shuleni linaendelea kujitokeza, baada ya kuwapo kwa idadi kubwa wanafunzi kupata ujazito, katika kipindi cha mwaka 2021/2022.

Kwa mujibu wa Naibu Waziri akiwa bungeni jijini Dodoma Januari mwaka huu, katika kipindi cha mwaka 2021 na 2022 wanafunzi 9,011 za shule za msingi na sekondari walipata mimba.

Anafafanua kuwa wanafunzi 1,554 ni wa shule za msingi na 7,457 wa shule za sekondari walipata ujauzito, ambapo takwimu hizo zinamshtua Spika wa Bunge, Dk. Tulia Ackson na kuitaka wizara kuandaa takwimu za idadi ya walioshtakiwa kwa kupatikana na hatia ya kuwapa ujauzito wanafunzi.

Katika maelekezo yake, Dk. Tulia anasema takwimu kuhusu wanaume wenye hatia ni muhimu, ili kusaidia kuona kama sheria ya kuwalinda watoto dhidi ya vitendo viovu inafanya kazi na kuleta matokeo chanya.

**SAMIA SCHOLARSHIP**

Nchi nyingi duniani zinazoendelea ni zile ambazo zimejikita katika ubunifu, kwenye utafutaji maendeleo ya wananchi wake, kutokana na ukweli kwamba, ubunifu ni nguzo kuu ya kufanikisha maendeleo.

Kwa kuzingatia hilo, Rais Samia naye ameamua kuelekeza nguvu zake huko, kwa kuanzisha ufadhili wa masomo ya sayansi kupitia programu iitwayo (SAMIA SCHOLARSHIP 2022/2023), kwa wanafunzi wenye ufaulu mzuri.

Tayari serikali ilishatenga Sh. bilioni 3, kwa ajili ya programu hiyo ya kuwasomesha wanafunzi waliopata ufaulu wa juu, katika masomo ya sayansi kwenye mitihani yao ya kidato cha sita.

Vilevile, majina 640 ya wanafunzi wanaokidhi vigezo vya kuomba ufadhili huo yalishatangazwa na Waziri wa Elimu, Sayansi na na Teknolojia, Profesa Aldof Mkenda jijini Dodoma Septemba mwaka jana.

"Wote ambao watahitimu chini ya Samia Scholarship watakuwa na uwezo wa kuomba mkopo na watapatiwa, ili kujiendeleza kimasomo. Ubunifu ni nguzo muhimu, Rais ameamua kuwekeza huko," Prof. Mkenda anasema.

Kwa hatua hiyo, ni wazi kwamba katika kipindi chake cha miaka miwili madarakani, Rais amedhamiria kuhakikisha elimu inaimarika zaidi ikiendana na teknolojia na ubunifu wa vitu mbalimbali.

Serikali imekuwa ikikutana na wataalamu wa elimu kutoka sehemu mbalimbali ili kubadilishana ujuzi na maoni ya jinsi ya kuangalia mitaala ili iendane na soko la ajira kidunia na pia kuhakikisha elimu inatoa ujuzi kwa wahitimu.

**UBORESHAJI SHULE**

Tangu aingie madarakani, Rais amejitahidi kuboresha miundombinu ya shule kuanzia ujenzi wa madarasa, uongezaji wa madawati katika shule za msingi na sekondari ili kuepusha wanafunzi kukaa chini au kusomea chini ya miti.

Katika mwaka wa fedha 2021/2022, serikali kupitia fedha za UVIKO- 19 ilielekeza Sh. bilioni 300, kwa ajili ya kujenga madarasa 12,000 katika shule za sekondari na madarasa 3,000 kwa shule shikizi.

Aidha, serikali ilitoa Sh. bilioni 160, kujenga madarasa 8,000 nchi nzima, huku kupitia mradi wa kuimarisha elimu ya sekondari nchini (Sequip) zikitolewa Sh. trilioni 1.2 ambapo Sh. bilioni 143.47 zilikuwa zimeshatumika katika ujenzi wa shule 232 katika mwaka wa fedha 2021/22.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Angela Kairuki ndiye anayesema hayo na kufafanua kuwa katika mwaka wa fedha 2022/23 serikali itajenga shule 184 za sekondari katika halmashauri zote.

"Kila shule itagharimu shilingi milioni 600, lengo la serikali ni kutaka kuhakikisha hakuna kata ambayo itakuwa haina shule ya sekondari. Tunamshukru Rais Samia kwa kuchagiza maendeleo kwenye sekta ya elimu," anasema Angela.

Pamoja na hayo anasema kwa miaka mitano ijayo, serikali itajenga shule 1,026 kupitia mradi wa Sequip na kupitia mradi wa kuboresha elimu ya awali na msingi itaboresha madarasa zaidi ya 9,000 yenye thamani ya Shilingi bilioni 250.9.

Kwa ujumla ni kwamba, miaka miwili ya Rais Samia madarakani, serikali imejitahidi kuhakikisha inaboresha elimu katika ngazi mbalimbali kuanzia elimu ya awali hadi vyuoni.

ELIMU

NA DK FELICIAN B. KILAHAMA

# Ushoga na ndoa za jinsi moja unavyopingana na maumbile



Amir Ohana, Spika wa Bunge la Israel –Knesset, anayetetea ndoa za jinsia moja. **PICHA: KNESSET**

USHOGA siyo neno geni kwa Watanzania licha ya kwamba miaka iliyopita matumizi yake yalikuwa tofauti na ilivyo leo.

Ikumbukwe kabla ya kupata uhuru na baada ya kujitawala hadi miaka ya 1990, ungeweza kusema kipindi hicho ni 'majira ya zamani', lakini kuanzia miaka ya 1990 hadi leo 2023 kukiita kipindi cha majira ya sasa ni sahihi.

Iwe zamani au sasa masuala ya sayansi na teknolojia; mila, desturi, utamaduni, siasa na mazingira husuan mabadiliko ya tabianchi hayakwepeki kwa kumaanisha kwamba ni mambo yanayojitokeza katika vipindi vyote viwili utofauti ni kiwango cha kasi yanayokuja nayo,

Mathalani, sayansi na teknolojia hata zamani vitu hivyo vilikuwapo ila kiwango cha mabadiliko kimeonekana kushika kasi zaidi katika miongo mitatu iliyopita au zama hizi ama majira ya sasa.

Kadhalika kwenye masuala ya kijamii, utamaduni, mila na desturi nazo zina mabadiliko makubwa, mfano, mambo ya mila potofu na kandamizi hasa kwa wanawake na watoto zimeendelea kutoweka.

Masuala machache kama 'ukeketaji' na baadhi ya wazazi kutopenda watoto wao wapate elimu pamoja na serikali kuamua watoto wasome bure mpaka kidato cha sita, lakini hali bado ni 'kizungumkuti'. Katika siasa pia kumekuwapo na mapya vipo vyama vingi. Zamani, msingi ulikuwa wa chama kimoja pamoja na falsafa na itikadi za Ujamaa na Kujitegemea zilizojengwa kwenye msingi wa binadamu wote ni sawa na Afrika ni moja na kuzingatia 'utu' na 'heshima' kwa binadamu wote bila ya kuwapo kubaguana.

Hali ya mazingira ukilinganisha zamani na sasa kasi ya kubadilika imekuwa kubwa nyakati hizi masuala mengine yameibuka na kutishia heshima ya binadamu.

Mathalani, mihemko na kushabikia, kwa kiasi kikubwa, uhusiano hata ndoa za jinsia moja.

Mambo kama haya yanasababisha kutokuelewana katika familia nyingi, jamii na taifa kwa ujumla kwa sababu yanagusa zaidi imani, maadili na misingi ya uumbaji wa wanadamu ambao ni mume na mke. Inafika mahali wengi wanajiuliza kulikoni katika majira haya ya sasa, wanaume kuoana?

Kwa miongo miwili iliyopita suala hili limekuwa likipigiwa gitaa kwa sauti kubwa ili wahusika kujinafasi wapendavyo. Katika Kamusi ya Kiswahili Sanifu; Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili, Chuo Kikuu cha Dar-es-Salaam (1981) inabainisha kuwa 'shoga' ni jina linalotumiwa na wanawake walio-marafiki sana wakati wa kuitana au kujulishana kwa wengine.

Mfano, fulani ni shoga yangu kwa kumaanisha rafiki yake wa karibu neno likitumiwa zaidi mijini na kuzoeleka kwa kuhusishwa na kinamama walioshibana.

Vilevile, kamusi hiyo inabainisha kuwa 'shoga' ni aina ya mwanamume anayefanya mambo ya kike au kuashiria ni mwanamume asiye na uwezo wa kufanya tendo la ndoa.

Kadhalika, kamusi ya Kiingereza: inamtaja mwanamume anayefanya mambo ya kike kuwa ni 'gay' kumaanisha wanaume ambao wanavutiwa kufanya mapenzi ya jinsia moja.

Kwa lugha hiyo mwanamke anajulikana ni 'lesbian' hivyo, 'gay' na 'lesbian' ni wanaume na wanawake wanaohangaika na uhusiano wa mapenzi ya jinsia moja na kwa pamoja kujulikana kama 'homosexuals'.

> Kutokana na hatua hiyo, watu wakamjua Mungu wa kweli na kuachana na maagano au ibada za kijadi na kimila. Katika kumjua Mungu wa kweli, ndipo pia tulipofahamu kuwa alimuumba binadamu kwa mfano na sura yake:

Hii ni hali au dhana inayopingana na mahusiano ya watu wa jinsi tofauti yaani 'mume' na 'mke' kama ilivyoainishwa tangu kuumbwa kwa binadamu wa kwanza, Adam na Hawa au Eva.

Tangu uumbaji urafiki kwa watu wa jinsi moja ulikuwapo na kwamba watu wapendane, kama Mungu mwenyewe anavyowapenda. Hivyo, kulikuwa na upendo na hata sasa inatakiwa iwe hivyo kutokana na agizo la kupendana kama ndugu ambao ni sehemu ya uzao wa Adam na Hawa.

Sasa dunia imechafuka yanayozuka sasa yanaashiria hali ilivyo ya machafuko na yeye asili ya kishetani, kinachoshangaza ni chimbuko la machafuko haya kutokana na mataifa yenye maendeleo makubwa ya elimu, sayansi na teknolojia na utandawazi wa hali ya juu.

Mataifa kama Tanzania yanakazana kujiletea maendeleo (kwa kurejea yaliyofanyika katika nchi zilizoendelea sana).

Kimsingi, baadhi ya mataifa hayo yametawala Bara la Afrika, katika harakati za kutawala, wakaanzisha shule ili kuwe na elimu na kuongeza maarifa. Kadhalika, wakaanza kujenga baadhi ya miundombinu kama Reli ya Kati: Dar-es-Salaam mpaka Mwanza na Kigoma pia mpaka Mpanda mkoni Katavi. Vilevile, wakajenga bandari, barabara na huduma za afya mfano, hospitali na vituo vya afya na zahanati.

Juhudi hizo zililenga kuandaa Watanzania wakati ule Watanganyika na Wazanzibari, kuweza kumudu maisha kwa kuwa na afya njema, akili na maarifa na kufanya maamuzi sahihi.

Haikupita muda mrefu, Wamisionari kutoka mataifa yaliyoendelea wakafika nchini zaidi ya miaka 100 iliyopita kwa kusudi za kueneza injili ambayo ni habari njema kwa watu wote.

Kutokana na hatua hiyo, watu wakamjua Mungu wa kweli na kuachana na maagano au ibada za kijadi na kimila. Katika kumjua Mungu wa kweli, ndipo pia tulipofahamu kuwa alimuumba binadamu kwa mfano na sura yake:

Akamfanya mtu kwa mavumbi ya ardhi, akampulizia pumzi ya uhai baada ya kumuumba Adam, Mungu akaona amekuwa mpweke; akasema 'si vema huyo 'mtu' awe peke-yake, nitamfanyia msaidizi wa kufanana naye'.

Ndipo Bwana Mungu akamletea Adam usingizi mzito, kisha akatwaa ubavu wake mmoja akafunika nyama mahali pake na ule ubavu alioutwaa katika Adamu, akaufanya mwanamke akamleta kwa Adam. Hivyo, Mungu akaumba jinsia mbili ya kiume na kike na Adam akawa mzaliwa wa kwanza wakati huo msaidizi wake akawa mzaliwa wa pili.

Mungu akawabariki akawaambia zaeni mwongezeke na kuijaza nchi: mzaliwa wa kwanza Adam' akapewa amri ya kumiliki na kutawala na kuisimamia familia yake ipasavyo wakati huo mzaliwa wa pili Hawa akiwa msaidizi wake halisi.

### NI HAPANA USHOGA

Kwa msingi huo Mwenyezi Mungu ndiye asili na msingi wa familia zote; mwanamume aishi na mwanamke na wazae na kuongezeka zawadi ya watoto kutoka kwa muumbaji wao.

Kwa kuwa Hawa alitwaliwa katika mwanamume, hivyo mwanamume atawaacha wazazi wake baba na mama, naye ataambatana na mkewe na watakuwa mwili mmoja. Sasa taswira za mwanamume kumuoa 'mwanamume' au mwanamke kumuoa mwanamke zinatoka wapi? Hilo ni vyema lisikubalike. Dunia itakuwa jangwa kukowapi kuzaa na kuongezeka kama Mungu alivyowaagiza? Binadamu na Watanzania tafakarini njia zenu.



## W'biashara sokoni watakiwa kuchagua viongozi bora

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

DIWANI wa Kata ya Chamwino jijini Dodoma, Jumanne Ngede, amewataka wafanyabiashara katika masoko kutowachagua viongozi wanaohamasisha migogoro isiyo na tija.

Ngede alibainisha hayo juzi wakati akizungumza na wafanyabiashara wa Soko la Bonanza jijini hapo, kwenye mkutano mkuu wa uchaguzi wa viongozi wao.

Alisema wafanyabiashara hao wanapaswa kuwa makini wanapowachagua viongozi ili wasijute kwa kipindi chote watakachokuwapo madarakani.

"Niwaombe wafanyabiashara wa Bonanza chagueni viongozi watakaoshirikiana na serikali katika kuwaletea maendeleo na siyo wale wanaohamasisha migomo au kwa kufuata sura, kabila, rangi, hapo mkikosea tu mtajuta kwenye kipindi chote watakachokuwa madarakani,"alisema.

Pia aliwahimiza kuchagua viongozi ambao watakuwa mstari wa mbele katika kuibua miradi mbalimbali kwa ajili ya maendeleo ya wafanyabiashara na waaminifu.

Ngede alisema amekuwa akiwahamasisha viongozi wa soko hilo kufanya kazi zao kwa uaminifu, sambamba na kuitisha mikutano kwa ajili ya kusoma mapato na matumizi ya wafanyabiashara wa soko hilo.

Alisema kuwa viongozi wakiwa na tabia ya kukutana watawajengea uaminifu kwa wafanyabiashara kwa kuwa watakuwa wabunifu wa miradi mbalimbali ambayo itakayo wawezesha kupata hata na mikopo.

Mwenyekiti wa Kata ya Chamwino, Lucas Nkelege, alisema hatakuwa tayari kufanya kazi na viongozi wanaopingana na juhudi za serikali sambamba na wale ambao wanaohamasisha migomo.

**Ngede alibainisha hayo juzi wakati akizungumza na wafanyabiashara wa Soko la Bonanza jijini hapo, kwenye mkutano mkuu wa uchaguzi wa viongozi wao.**

# Bunge laiagiza TACAIDS kuzifuatilia kamati za UKIMWI

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

TUME ya Kudhibiti Ukimwi Tanzania (TACAIDS), imeagizwa kufanya ufuatiliaji wa utekelezaji wa majukumu ya kamati za kudhibiti UKIMWI ngazi za chini ili zisifanye kazi kwa mazoea.

Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Afya na Masuala ya Ukimwi, Stanslaus Nyongo, alitoa maelekezo hayo baada ya tume hiyo kuwasilisha taarifa kuhusu muundo na majukumu yake kwa kamati hiyo jijini hapo.

Pamoja na mambo mengine Nyongo aliipongeza TACAIDS kwa kazi waliyoifanya katika kudhibiti na kupunguza maambukizi ya Virusi Vya Ukimwi (VVU) nchini na kiagiza kuendelea kufanyia kazi ushauri na maekezo yaliyotolewa na kamati hiyo.

Naye Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge na Uratibu, George Simbachawene, alisema serikali kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu itaendelea kutoa ushirikiano unaostahiki kwa kamati hiyo kwa kufuata miongozo, maoni na ushauri.

Awali akiwasilisha taarifa ya muundo wa tume hiyo, Mkurugenzi Mtendaji wa TACAIDS, Dk. Leonard Maboko, alitaja majukumu ya TACAIDS kuwa ni kuandaa sera na miongozo kwa ajili ya mwitikio wa UKIMWI nchini pamoja na kusimamia athari zake.

Alibainisha kuwa TACAIDS pia inakuza uraghibishi na utoaji wa elimu kwa ngazi ya juu kuhusu kuzuia na kudhibiti UKIMWI pamoja na kufuatilia na kutathmini shughuli zote za ugonjwa huo zinazotekelezwa nchini.

Alitaja jukumu lingine ni kuhamasisha haki na wajibu kwa watu wanaoishi na VVU waishi kwa matumaini na kuishauri serikali kuhusu masuala yote yanayohusu kuzuia na kudhibiti UKIMWI.

Pia kutambua vikwazo katika utekelezaji wa kuzuia na kudhibiti katika sera na programu.




Wananchi kutoka maeneo mbalimbali Wilaya ya Chamwino mkoani Dodoma, wakiwa nje ya jengo la ofisi za Kijiji cha Chamwino kwenye foleni wakisubiri kununua mahindi ya bei nafuu yanayotolewa na serikali, kilo 25 kwa Sh. 19,500. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Kamati ya Bunge kukagua miradi Ofisi ya Waziri Mkuu

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

KAMATI ya Bunge ya Ustawi na Maendeleo ya Jamii inatarajia kukagua utekelezaji wa miradi mitano inayotekelezwa na Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Ajira, Vijana na Wenye Ulemavu na taasisi zilizo chini yake.

Miradi hiyo ni ujenzi wa kiwanda cha sukari Mkulazi, machinjio ya kisasa Nguru Hills, ukarabati wa kiwanda cha chai Mponde, Chuo cha Ufundi kwa watu wenye ulemavu cha Masiwani na ujenzi wa vitalu nyumba mkoani Arusha.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Ajira, Vijana na Wenye Ulemavu, Prof. Joyce Ndalichako, alieleza hayo alipokuwa akiwasilisha taarifa ya utekelezaji wa miradi hiyo.

Prof. Ndalichako alisema ratiba ya shughuli za kamati inaonyesha kamati hiyo itaanza kutembelea na kukagua miradi hiyo leo.

Alisema kwa mradi wa ujenzi wa kiwanda cha sukari Mkulazi unaomilikiwa na Mfuko wa Hifadhi ya Taifa (NSSF) umefikia asilimia 89 na uzalishaji unatarajiwa kuanza Julai mwaka huu.

Alisema mradi wa machinjio ya kisasa ya Nguru Hills Wilaya ya Mvomero mkoani Morogoro unaomilikiwa na PSSSF utazalisha ajira za moja kwa moja zisizopungua 350 na zaidi ya ajira 2,000 zitakazotokana na mnyororo wa thamani.

Prof. Ndalichako alisema mradi huo utakuwa na uwezo wa kuchinja ng'ombe 100 na mbuzi 1,000 kwa siku na Kampuni ya Nguru itanunua mifugo kutoka kwa wafugaji.

Kuhusu kiwanda cha chai, Prof. Ndalichako alisema tayari kimeanza kufanya kazi na kilo 24,460 zimeuzwa na tani 50 zinategemewa kuuzwa Machi mwaka huu, 2023.

Akizungumzia Chuo cha Masiwani, Waziri Ndalichako alisema ni miongoni mwa vyuo sita vilivyo chini ya ofisi hiyo kinachotoa elimu ya uzalishaji mali na kinamsaidia mtu mwenye ulemavu kwa kumfundisha mbinu za marekebisho ya viungo ili kumwezesha kufanya kazi mbalimbali.

Kadhalika, alisema katika ujenzi wa vitalu nyumba upo chini ya Programu ya Taifa ya Kukuza Ujuzi na Vijana 12,580 kutoka halmashauri 117 za mikoa 17 nchini wamenufaika na mafunzo ya kilimo cha kisasa kwa kutumia teknolojia ya kitalu nyumba. Aliahidi ofisi hiyo itaipa kamati hiyo ushirikiano ili kuishauri serikali masuala mbalimbali ya utekelezaji wa miradi hiyo ya maendeleo.

Mwenyekiti wa kamati hiyo, Fatuma Toufiq alipongeza ofisi hiyo kwa utekelezaji wa miradi hiyo na kuahidi kushirikiana ili kutoa ushauri kwa serikali utakaoleta tija zaidi.

Katibu Mkuu wa ofisi hiyo, Prof. Jamal Katundu, alisema ofisi hiyo ndiyo yenye jukumu la kuratibu fursa za ajira ili kutekeleza ilani ya uchaguzi ya CCM ya mwaka 2020-2025 iliyoahidi ajira milioni nane zitengenezwe kwa kipindi hicho.





# RC awapa maagizo makamanda wa polisi Nyanda za Juu Kusini

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

MAKAMANDA wa Jeshi la Polisi mikoa ya Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, wametakiwa kuandaa mpango wa pamoja wa kudhibiti matukio ya uhalifu, ikiwamo kukabiliana na biashara haramu ya usafirishaji binadamu.

Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera, alitoa agizo hilo mwishoni mwa wiki alipokuwa anafungua mkutano wa pamoja wa wakuu wa vyombo vya ulinzi na usalama wa mikoa mitano ya Kanda ya Nyanda za Juu Kusini.

Mkutano huo uliwashirikisha makamanda wa polisi wa mikoa, wakuu wa magereza, wakuu wa vikosi vya usalama barabarani wa mikoa, wakuu wa hifadhi za taifa na maofisa uhamiaji kutoka katika mikoa hiyo.

Maofisa walioshiriki mkutano huo walikuwa ni kutoka katika mikoa ya Iringa, Njombe, Mbeya, Songwe na Rukwa ambao walikutana kwa lengo la kujadili kwa pamoja mbinu za kukabiliana na matukio ya uhalifu.

Homera alisema tatizo kubwa ambalo linaikabili mikoa hiyo ni usafirishaji haramu wa binadamu hasa raia wa Ethiopia na Somalia ambao alisema wamejaa kwenye magereza ya Mkoa wa Mbeya.

Alisema wahamiaji hao wamekuwa wakivuka mikoa mbalimbali lakini wanakwenda kukamatiwa Mbeya jambo ambalo alisema linamtia wasiwasi kwamba kuna baadhi ya maofisa hawawajibiki vizuri kwenye mikoa yao.

"Mpaka sasa kwenye gereza letu hapa Mbeya Waethiopia na Wasomali wapo 284, lakini hapa kuna mikoa ya Njombe na Iringa kwanini waje wakamatwe Mbeya kwamba huko kwingine wanapaa angani?" Alihoji Homera.

Aidha, aliwataka wakuu wa hifadhi za taifa kuimarisha ulinzi kwenye maeneo yao ili kudhibiti vitendo vya ujangili ambavyo vimekuwa vikishamiri kwenye hifadhi.

Alisema majangili wamekuwa wakiingia hifadhini na kuua wanyama kwa ajili ya kupata kitoweo na nyara zingine za serikali.

Alisema hivi karibuni waliwakamata watu wawili wilayani Mbarali wakiwa na nyama ya twiga ambaye walimuwinda kwenye Hifadhi ya Taifa ya Ruaha.

Akizungumza kwa niaba ya makamanda wa polisi wa mikoa hiyo, Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Njombe, Kamishna Msaidizi wa Polisi, Hamis Issa, alisema waliamua kufanya mkutano huo kutokana na kushamiri kwa matukio ya uhalifu.

Alisema asilimia kubwa ya makosa ambayo yamekuwa yakitokea yanavuka mipaka kutoka katika mkoa mmoja kwenda mwingine na hivyo udhibiti wake unahitaji ushirikiano.

"Lengo letu hapa ni kuhakikisha tunakuwa na mpango mkakati wa pamoja wa kukabiliana na matukio haya kwenye mikoa yetu ili wananchi wetu waishi kwa amani," alisema Kamanda Issa.

Aliwataka wananchi kutoa ushirikiano kwa Jeshi la Polisi katika kukabiliana na matukio ya uhalifu kwa kuhakikisha wanatoa taarifa za uhalifu ili wadhibitiwe kabla hawajatekeleza uhalifu huo.

Alisema yanapotokea matukio ya uhalifu wanaoathirika zaidi ni wananchi wa kawaida na hivyo akawataka kushiriki katika kudhibiti vitendo hivyo.



Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera (katikati), akiagana na wakuu wa vyombo vya ulinzi na usalama wa mikoa ya Nyanda za Juu Kusini wakati wa kikao cha pamoja cha kujadili namna ya kukabiliana na matukio ya uhalifu mwishoni mwa wiki, kushoto ni Mkuu wa Wilaya ya Mbeya, Beno Malisa. **PICHA: NEBART MSOKWA**

## TEMESA yatupiwa lawama kushindwa kutoa huduma bora

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WAKALA wa Ufundi na Umeme (TEMESA) umelalamikiwa na wadau mbalimbali kwa kushindwa kutoa huduma bora hususani za ufundi.

Malalamiko hayo yalitolewa na wadau wa TEMESA kutoka katika maeneo mbalimbali ya Mkoa wa Mbeya ambao walisema taasisi hiyo haitekelezi vizuri majukumu yake kama ambavyo serikali inakusudia.

Mmoja wa wadau hao, John Meshack ambaye ni Msimamizi wa Shule ya Maadilisho ya Ilambo alisema vipuli ambavyo vinatumiwa na taasisi hiyo vinakuwa siyo bora.

Vilevile alisema mafundi wa taasisi hiyo hawaendani na teknolojia ya kisasa hali ambayo inawafanya watengeneze vyombo vya moto kwa kiwango cha chini.

"Sisi ni wateja wa muda mrefu wa taasisi hii lakini tumekuwa haturidhiki na ufundi wao, kinachotulazimisha kwenda kwao huwa ni sheria," alisema Meshack.

Ofisa kutoka Benki ya Kilimo Tanzania (TADB), James Mwanyayo, alisema magari yanayopelekwa TEMESA kwa ajili ya matengenezo huwa yanakaa muda mrefu hali ambayo inakwamisha shughuli zao.

Alishauri taasisi hiyo kuongeza nguvu kazi hasa mafundi ili kazi za matengenezo ya magari zifanyike kwa haraka kuepuka kukwamisha shughuli za wadau.

Mkurugenzi wa Matengenezo na Huduma za Ufundi wa TEMESA, Mhandisi Hassan Karonda, alisema wameanza mikakati ya kuboresha huduma ili kupunguza malalamiko ya wadau.

Alisema moja kati ya maboresho waliyoyafanya ni pamoja na kuingia mikataba na baadhi ya kampuni yanayouza vipuri ili wapate vifaa vya kisasa.

Alisema lengo la kuingia mikataba na kampuni hizo ni kupunguza mchakato wa manunuzi ambao ndiyo umekuwa ukichelewesha matengenezo.

# Programu uboreshaji thamani kahawa, chai waleta neema

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

PROGRAMU ya uboreshaji wa mnyororo wa thamani wa kahawa, chai na mazao ya bustani ijulikanayo kwa jina la AGRI-CONNECT imeanza kuleta manufaa kwenye kilimo cha kahawa katika mikoa ya Kanda ya Nyanda za Juu Kusini.

Programu hiyo inatekelezwa katika mikoa ya Mbeya, Iringa, Njombe, Songwe na Ruvuma ambapo inatekelezwa kwa ufadhili wa Jumuiya ya Umoja wa Ulaya (EU).

Meneja wa Taasisi ya Utafiti wa Kahawa nchini (TacRI), Nyanda za Juu Kusini, Dismas Pangalas, aliyasema hayo mwishoni mwa wiki wakati wa ziara ya kukagua utekelezaji wa miradi mbalimbali ya programu hiyo.

Maofisa walioshiriki kwenye ziara hiyo ni wawakilishi wa EU, maofisa kutoka katika wizara mbalimbali zinazotekeleza miradi hiyo, watekelezaji wa miradi pamoja na vyama vya ushirika vya wakulima wa kahawa.

Maofisa hao walifanya ziara katika halmashauri za Mbeya na Rungwe zilizoko katika Mkoa wa Mbeya pamoja na Halmashauri ya Wilaya ya Mbozi mkoani Songwe. Pangalas alisema wamekuwa wakishirikiana na AMCOS mbalimbali kuzalisha miche ya kisasa ya kahawa ambayo imefanyiwa utafiti na kuigawa kwa wakulima kulingana na makubaliano ya wanachama.

Alisema miche ambayo wanaizalisha ni aina ya compact ambayo ina tija kuliko aina zingine za kahawa ambazo wakulima wamekuwa wakiilima miaka yote.

"Katika ukanda huu wa Umalila tunafanya kazi na AMCOS mbili ambazo ni Umalila Amcos na Shizingo Amcos, kwa mwaka huu Shizingo wamezalisha miche 33,000 na Umalila wamezalisha miche 34,010," alisema Pangalas.

Alisema mbali na kuwasaidia wakulima kuzalisha miche hiyo lakini wamekuwa wakiwapatia elimu ya uzalishaji wa miche hiyo ya kisasa.

Katibu wa Shizingo AMCOS, Ntuta Wilson, alisema chama chake kina wanachama 400 ambao wote ni wakulima wa kahawa na kwamba mbali na wanachama hao pia wanawahudumia wakulima wengine 150.

Alisema aina ya miche ambayo wanaitumia kwa sasa ina tija kubwa kuliko ya asili ambayo wamekuwa wakiitumia na kwamba hali hiyo imesababisha mwamko wa wakulima kuongezeka.

Mkurugenzi Mkuu wa Bodi ya Kahawa nchini, Prims Kimario, alisema programu hiyo ya AGRI-CONNECT mbali na kuongeza tija kwenye uzalishaji wa kahawa pia hata ubora wa zao hilo umeongezeka.

Alisema katika ziara hiyo walibaini kwamba wakulima bado wanakabiliwa na baadhi ya matatizo ikiwamo ukosefu wa maji na umeme kwenye vitalu vya miche na viwanda vidogo vya kuchakata zao hilo.

Ofisa Programu wa EU, Andrea Maccarelli, alisema katika maeneo yote ambayo walitembelea waliridhika na utekelezaji wa programu hiyo hasa kwenye kilimo cha kahawa ambako wakulima wadogo wanashiriki.

Alisema jumuiya hiyo itaendelea kushirikiana na Tanzania katika kuboresha maisha ya wananchi hasa katika sekta ya kilimo ambayo ndiyo inasaidia kuzalisha chakula.



## SMZ yawahakikishia ushirikiano madaktari utoaji huduma

**Na Mwandishi Wetu**

SERIKALI ya Mapinduzi ya Zanzibar, imesema itaendelea kuunga mkono jitihada zinazochukuliwa na madaktari wazalendo katika kuwapatia huduma za afya wananchi katika maeneo mbalimbali.

Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Hemed Suleiman Abdulla, aliyasema hayo katika hafla ya kuwashukuru madaktari wazalendo.

Alisema serikali itaendelea kuthamini juhudi zinazochukuliwa na madaktari wazawa katika kuwapatia huduma za afya wananchi.

Alisema katika kuimarisha upatikanaji wa huduma za afya, serikali iko katika hatua za mwisho za kukamilisha ujenzi wa hospitali za kisasa kila wilaya na kwamba zitapatiwa vifaa stahiki pamoja na watumishi wanaohitajika ili zitoe huduma bora kwa wananchi.

Aidha, alisema hivi karibuni serikali imepitisha sera ya kuanzisha mfuko wa bima ya afya, hali ambayo itarahisisha upatikanaji wa huduma hizo kwa wananchi.

Kadhalika aliwashukuru wafadhili waliochangia katika kufanikisha bonanza hilo akiwamo mmiliki wa hoteli ya Ngalawa, Shirika la Bima la Zanzibar, Izmir, Wizara ya Afya, pamoja na Mamlaka ya Mapato Zanzibar.

Katika kuonesha kuunga mkono, Makamu wa Pili wa Rais, alichangia Sh. milioni 10 ambazo zitasaidia huduma za afya katika bonanza hilo.

Sambamba na hayo Hemed aliupongeza uongozi wa Mkoa wa Kaskazini Unguja kwa kuandaa bonanza hilo ambalo linalenga kuimarisha afya za wananchi wa mkoa huo.

Waziri wa Afya, Nassor Ahmed Mazrui, alisema kupitia bonanza hilo wizara imejifunza mambo mbalimbali na itahakikisha inashirikiana na wadau wa afya katika utoaji huduma bora kwa wananchi wote.

Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini Unguja, Ayoub Mohammed Mahmoud, alisema kupitia bonanza hilo mkoa umefanikiwa kutoa huduma za afya bora kwa wananchi.

Alisema wananchi 9,195 wamepimwa afya na kupatiwa matibabu, ambapo pia chupa 349 za damu salama zimepatikana, huku wananchi 114 wamechanja chanjo ya corona na wananchi 210 wamepatiwa matibabu ya macho.

**Katika kuonesha kuunga mkono, Makamu wa Pili wa Rais, alichangia Sh. milioni 10 ambazo zitasaidia huduma za afya katika bonanza hilo.**

# PBZ, Asma watoa msaada wa vifaa tiba kwa wajawazito

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

BENKI ya Watu wa Zanzibar (PBZ) kwa kushirikiana na Taasisi ya Asma wamekabidhi msaada wa vifaa tiba kwa wajawazito na watoto katika Hospitali ya Makunduchi iliyoko Mkoa wa Kusini Unguja.

Akizungumza jana baada ya kukabidhi vifaa hivyo, Mkurugenzi wa Biashara kutoka PBZ, Eddie Mhina, alisema vifaa vilivyotolewa vitasaidia kuimarisha afya za wajawazito na watoto waliozaliwa.

Alisema kuna umuhimu wa kutoa vifaa hivyo kwa sababu wanatambua mchango mkubwa na umuhimu wa kinamama katika kuchangia shughuli za maendeleo ya nchi.

Mhina alisema licha ya PBZ kuwa taasisi ya kifedha bado wana wajibu wa kushirikiana na serikali katika kuisaidia jamii kwenye nyanja mbalimbali.

"Mpango wa PBZ ndani ya kipindi hiki ni kuimairisha huduma za kifedha kupitia matawi mbalimbali yanayoadhimishwa kuweka vifaa vya kisasa, ili kuwasaidia wananchi kupata huduma hiyo kwa urahisi na haraka,"alisema.

Mwanzilishi wa Taasisi ya Asma, Asma Mwinyi, alisema msaada huo utawasaidia kinamama wanapojifungua wawe salama.

Alisema kinamama wengi hukumbwa na matatizo mbalimbali wakati wa kujifungua, hivyo kupatikana kwa msaada huo utaokoa vifo vyao.

Naye Muuguzi Mkuu wa wodi ya kinamama na watoto hospitalini hapo, Wadhiha Ambar Maftaha, alisema msaada huo utasaidia kukidhi mahitaji ya kinamama wakati wa kujifungua.

Alisema uamuzi wa taasisi hizo kutoa msaada huo kwa makundi hayo inaonyesha ni jinsi gani inavyowajali kinamama na watoto katika kuimarisha ustawi wa afya zao.

Sheha wa Shehia ya Mzuri Makunduchi, Hamza Issa, alisema: "Wanaume wengi, wake zao wanapokuwa wajawazito huwa hawakamilishi mahitaji yao ikiwamo vifaa tiba kwa ajili ya kujifungua".




Konda wa daladala njia ya Bububu hadi Darajani Unguja aliyefahamika kwa jina moja la Silima akiwa amevaa suti akiashiria kuipenda kazi yake na kuwa mfano kwa makonda wenzake wanaovaa hovyo katika kazi hiyo. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# ZIPA, kampuni za China zaingia makubaliano kutafuta wawekezaji

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

MAMLAKA ya Kukuza Uwekezaji Zanzibar (ZIPA) pamoja na Kampuni ya Shanghai Linghang Group na Weihai Huatan Supply China Management zimeingia makubaliano ya kufanya kazi kwa ajili ya kutafuta wawekezaji kuja Zanzibar.

Hatua hiyo imekuja ikiwa ni siku chache baada ya Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi kuzindua programu ya uwekezaji kwa njia ya kielektroniki.

Akizungumza baada ya utiaji wa saini makubaliano hayo, Mkurugenzi Mtendaji wa ZIPA, Shariff Ali Shariff, alisema makubaliano hayo yataongeza wigo wa kiutendaji katika kufikia wawekezaji wengi China. Alisema China ni kati ya nchi zilizowekeza Zanzibar na wanamchango katika pato la nchi, hivyo alizitaka kampuni hizo kufanya kazi kwa ufanisi, kwa kuongeza wawekezaji zaidi nchini na hasa katika sekta ya viwanda.

Mwenyekiti wa Kampuni ya Shanghai group ambaye ni mwakilishi wa Kampuni ya Weihai Huatan Supply, Lisa Wang aliishukuru ZIPA kwa kumpa fursa hiyo na aliahidi kufanya kazi kama makubaliano yanavyomwelekeza.

Msaidizi wa Kampuni ya Shanghai Group, Nassor Dachi, alisema uzinduzi wa uwekezaji kwa njia ya kielektroniki umefungua fursa kwa ZIPA kupata wawekezaji zaidi na mfumo huo utamfikia mwekezaji alipo.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA CHETI



**SHIDA M MWENDESHA** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S4401/0018** kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia **IDAHINA SECONDARY SCHOOL** mwaka 2019. Kwa yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. POLISI TAARIFA: **DAR/KIJ/RB/94180/2023**

**WIZARA YA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI**
**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA WILAYA YA MASWA**
**LILILOPO MASWA**
**MAOMBI MAKUBWA NO. 65 YA MWAKA 2022**
**KATI YA**
**MADUHU CHARLES.................MLETA MAOMBI**
**(Administrator of Estate of the Late Charles Nhelya)**
**DHIDI YA**
**LIMBU SUPI............................1. MJIBU MAOMBI**
**KAHABI NKENGELE.................2. MJIBU MAOMBI**
**NHELYA CHARLES.....................3. MJIBU MAOMBI**

### WITO/TAARIFA

**Kwa LIMBU SUPI Popote alipo katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania**

Kwa kuwa mwombaji hapo juu amefungua maombi dhidi yako na mwenzako katika Baraza hili la wilaya ya Maswa, maelezo ya madai yanaweza kupatikana hapa Barazani. Unatakiwa kuleta hapa Barazani utetezi wako wa maandishi (WSD) kabla ya tarehe 15.03.2023.

Pia unajulishwa kuwa shauri hili limepangwa kutajwa siku ya tarehe 15.03.2023 saa 2:30 asubuhi mbele ya Mhe. J.T. Kaare Mwenyekiti, Baraza la Ardhi na Nyumba wilaya ya Maswa.

Na pia unafahamishwa kuwa iwapo utakaidi wito huu na kushindwa kuleta utetezi wa maandishi kwa muda uliopangwa, Baraza litalazimika kusikiliza shauri hili upande mmoja na kutoa maamuzi dhidi yako.

31.01.2022.

J.T.KAARE
MWENYEKITI BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA (W)
MASWA

**THE REGISTRATION OF DOCUMENT ACT (CAP 117 RE 2002)**
**CHANGE OF NAME BY DEED POLL**

**BY THIS DEED I, BUNONO JOHN BALIKUMWE,** Karagwe District - Kagera Region, Tanzania **DO HEREBY** absolutely renounce and abandon the use of fomer names **BUNONO J. JOHN, BUNONO B. JOHN and BUNONO JOHNSTONE JOHN** as appear on my **NIDA No. 19600502358210000127** in lie thereof do assume and adopt the name of **BUNONO JOHN BALIKUMWE.**

And in pursuant of such change of name as aforesaid do hereby DECLARE that at all times hereinafter in all records, deeds and instructions, in writing and in all action and proceeding and in all dealing and transactions and upon all occasions whatever use and sign the said names of **BUNONO JOHN BALIKUMWE** in lie of the said names **BUNONO J. JOHN, BUNONO B. JOHN** and **BUNONO JOHNSTONE JOHN** of renounced as aforesaid.

And **I HEREBY** expressly authorize and require all person and whatsoever at all times after the date hereof to designate and address me in the name of **BUNONO JOHN BALIKUMWE** only.

In **WITNESS THEROF, I, BUNONO JOHN BALIKUMWE** have abandoned my old names of **BUNONO J. JOHN, BUNONO B. JOHN** and **BUNONO JOHNSTONE JOHN** and I have set my hand this **07th day of March, 2023.**

This signed and delivered at Bukoba
by the said **BUNONO JOHN BALIKUMWE**
who is known to me personally ................
The latter is known to me personally
this **07th day of March, 2023.**

DEPONENT



BEFORE ME:
Name:
Signature:
Postal address P.O BOX
QUALIFICATION: COMMISSIONER FOR OATHS

## TANGAZO KUPOTEA OFA YA KIWANJA

**ZUHURA KONDO SALUM** anatangaza kupotelewa na Ofa ya Kiwanja namba 152 kitalu "RR" kilichopo Mwalugoye Manispaa ya Shinyanga. Kwa yeyote atakaiona atoe taarifa kituo cha Polisi kilichopo karibu au awasiliane na Zuhura Kondo Salum kwa simu namba **0766-970324.** Taarifa ya Polisi **SHI/SHI/RB/91653/2023.**

## KUPOTEA KWA HATI YA KUSAFIRIA



**MSAFIRI ELIAS SONDOGO** anatangaza kupotea kwa hati ya kusafiria yenye Namba **TAE 215106.** Iliyotolewa Dar es salaam **PCO** mwaka **2019.** Kwa Yeyote ataekaeiona atoe taarifa Kituo chochote cha polisi.
**POLISI TAARIFA: DAR/KIL/RB/93325/2023.**

## KUPOTELEWA NA CHETI



**ERIKA SALVIUS LUGONGO** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index number **S4671/0005/2018** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia **MAHANJE SEKONDARI** mwaka 2018. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **DAR/CEN/RB/93985/2023.**

## KUPOTEA KWA KADI YA BAJAJ

**JACKSON MARWA WANYANCHA** anatangaza kupotelewa na kadi ya bajaji yenye namba za usajili **MC. 871 BUA** aina ya **PIAGGIO.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi kilichopo jirani yake. Taarifa ya polisi. **KAH/TR/RB/189/2023.**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**HUMPHREY LINLEY CARTER** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari yenye namba za usajili **T 752 AAK TOYOTA LANDCRUISER.** Chassis No. **HDJ810070751.** Engine No. **1HD0130543.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha Polisi. Taarifa ya Polisi: **ARU/ARU/RB/94292/2023.**

## KUPOTELEWA NA CHETI



**MWAJABU NGELA** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index number **S413/034/1989** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia **KIBITI SEKONDARI** mwaka 1989. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **DAR/CEN/RB/80941/2023.**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**DANIEL SHEM ONYANGO** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya **TOYOTA HIACE** yenye namba za usajili **T 744 AEK.** Kwa yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
**Taarifa ya polisi**
**ARU/ARU/RB/59012/2023**

**FORM NO. 58**
**IN THE COURT OF DISTRIC T DELEGATE**
**OF MOROGORO**
**DISTRICT AT MOROGORO**
**PROBATE AND ADMINISTRATION**
**CAUSE NO 20 OF 2023**

**In Matter of the Estate of the Late**
**FLAVIAN PASKALI LOKI**
**By 1. JUMA OSWARD GWAMBA**
**2. .................................**

All Persons claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of probate (or latter of administration) is made to the above - named petitioner.

Objection to the grand should be field on or before the **20th** day of **March, 2023.**

Dated at **Morogoro**, this **13rd** day of **March, 2023**

RESEDENT MAGISTRATE
RESIDENT MAGISTRATE INCHARGE
DISTRICT COURT

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA**
**WILAYA YA MOROGORO**
**LILILOPO MOROGORO**
**MAOMBI NAMBA 8 YA 2023**
**LINDA GODLIVING MEENA...... MLETA MAOMBI**
**DHIDI YA**
**RAJABU ALLY MOHAMED......MJIBU MAOMBI**

### WITO KUITWA SHAURINI KWA
**RAJABU ALLY MOHAMED.**

Popote ulipo unaarifiwa ufike katika Baraza la Ardhi na Nyumba Wilaya ya Morogoro tarehe 11/4/2023 mbele ya Mwenyekiti M.Khasim wewe mwenyewe binafsi au utume mwakilishi wako bila kukosa ambapo maombi yamepangwa kutajwa. Endapo hautaudhuria maombi yatatajwa na kusikilizwa upande mmoja dhidi yako na kutolewa uamuzi.

Imetolewa kwa **MKONO** wangu na **MUHURI** wa Baraza leo tarehe 08 mwezi Machi 2023

M.Khasim
MWENYEKITI
BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA (W)
MOROGORO


**OFISI ZA MATANGAZO**

*Mikocheni Industial Area,*

*Po.Box 31042, Dar es Salaam.*

*Mobile: +255 - 745 700 710.*

*E-mail: advertise@guardian.co.tz*

*Website: www.ippmedia.com*

*Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie 0677020701*

**TAHADHARI:** Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji **THE GUARDIAN LIMITED** hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

HABARI KIMATAIFA

## UN yasisitiza kufanyika mazungumzo DRC

**KINSHASA,** DRC

WAJUMBE wa Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa (UN) wametoa wito wa kufanyika kwa mazungumzo ya kumaliza ghasia zinazozidi kumwaga damu mashariki mwa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC).

Ujumbe huo wa Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa ulitoa wito huo jana baada ya kumaliza ziara ya siku tatu nchini humo.

Ujumbe wa mabalozi uliotumwa na Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa, ambao uliwasili DRC Jumanne ya wiki iliyopita, ulikutana na Rais Félix Tshisekedi mjini Kinshasa, na ulikwenda Goma na kukutana na viongozi wa eneo hilo na kutembelea kambi ya wakimbizi wa ndani.

Mjumbe wa ujumbe huo, Balozi wa Ufaransa katika Umoja wa Mataifa, Nicolas de Rivière, alisema kwamba M23 wanapaswa kujiondoa katika maeneo wanayoyashikilia na kuongeza kuwa "hakuna tena haja ya kuonyesha kwamba Rwanda inaunga mkono M23, mazungumzo pekee yanaweza kutatua mzozo huu".

"Njia ya kuondokana na mzozo huu inaweza tu kuwa ya kisiasa, na inaweza kupatikana tu kupitia mazungumzo," alisema.

Balozi wa Gabon katika Umoja wa Mataifa Michel Biang, alionyesha msisitizo kwamba diplomasia lazima itawale katika eneo hilo.

Inaelezwa kuwa ziara hiyo ilijiri baada ya kushindwa kwa usitishaji mapigano mashariki mwa DRC, uliojadiliwa na upatanishi wa Angola na kuvunjika siku ulipoanza kutekelezwa.

Inabainishwa kuwa mipango mingine kama hiyo ya amani imeshindwa huko nyuma hasa katika eneo la Mashariki mwa DRC, linalopakana na Rwanda, na kwamba limekuwa likikumbwa na kuzuka kwa ghasia tangu waasi wa M23 walipochukua silaha tena mwishoni mwa 2021, na kuteka maeneo yote ya eneo hilo.

Wapiganaji wa M23 pia walisonga mbele katika siku za karibuni, wakitishia kufunga barabara zote za kuingia Goma, jiji kuu la mashariki mwa DRC, karibu na Rwanda na ambalo lina zaidi ya wakazi milioni moja.

Mapigano kati ya majeshi ya Kongo na M23, ambayo DRC na mataifa mengine yanasema yanaungwa mkono na Rwanda, hadi sasa yamesababisha zaidi ya watu 800,000 kuyatoroka makazi yao kwa mujibu wa UN.

Hata hivyo ilielezwa kuwa mwishoni mwa wiki iliyopita, raia watano waliuawa kwa mashambulizi ya angani wakati wa mapigano kati ya vikosi vya Kongo na waasi wa M23 huko Kahumiro Goma. **RFI**

# Biashara silaha yatajwa kuongezeka Ulaya

**STOLKHOLM,** SWEDEN

TAASISI ya utafiti wa masuala ya amani duniani iliyoko Stolkholm, Sweden (SIPRI), imesema biashara ya silaha kwa ujumla duniani imepungua, lakini imeongezeka kwa kiwango kikubwa barani Ulaya.

Taasisi hiyo ya kimataifa hufanya utafiti na kulinganisha biashara ya silaha kwa kipindi cha miaka minne na ni kwasababu biashara ya silaha hubadilika badilika kila mwaka na kwa mtazamo wa taasisi hiyo utafiti wa muda mrefu ni bora zaidi katika kuakisi hali halisi ilivyo.

Mtafiti katika taasisi hiyo Pieter Wezeman, alizungumza na DW na kuyaweka wazi masuala muhimu yaliyojitokeza kwenye ripoti hiyo.

"Mabadiliko makubwa tuliyoyaona katika jukwaa la biashara ya silaha kimataifa, ikiwamo msaada wa kijeshi ni kwamba kwanza usafirishaji silaha katika nchi za Ulaya umeongezeka, lakini ni muhimu kusisitiza kwamba dhima ya Marekani kama msafirishaji mkubwa wa silaha kimataifa pia imeongezeka kwa kiwango kikubwa," alisema.

Aliongeza kuwa katika miaka ya hivi karibuni kuanzia 2018 mpaka 2022 biashara ya silaha kimataifa ilipungua kwa asilimia tano, ikilinganishwa na kipindi cha mwaka 2013 mpaka 2017.

Aidha, alieleza kuwa uagizaji silaha katika nchi za Umoja wa Ulaya (UK) na hususan kutoka Marekani uliongezeka kwa asilimia 47 na kwa nchi za Umoja huo ambazo ni wanachama wa Jumuiya ya kujihami NATO manunuzi ya silaha yaliongezeka kwa asilimia 65.

Pia alisema sababu ya ongezeko hilo barani Ulaya ni vita nchini Ukraine na kwamba nchi hiyo kwa sasa imekuwa ya tatu kati ya zinazopokea silaha kwa wingi duniani.

Alisema hiyo ni kwasababu nchi hiyo ambayo zamani ilikuwa chini ya muungano wa Kisovieti haikuwa na mahitaji makubwa ya silaha.

Hata hivyo, katika kipindi cha kuanzia mwaka 2018 mpaka 2022 nchi hiyo ilijikuta ikisimama katika nafasi ya 14 na kwamba mwaka 2022 pekee nchi hiyo ilikuwa katika nafasi ya tatu katika nchi zilizopokea silaha nyingi duniani.

Vile vile, alisema ripoti ya SIPRI inazungumzia kwa ujumla wake suala la biashara ya silaha ambayo pia inajumuisha msaada wa kijeshi kama ambavyo inashuhudiwa kufanyika kwa nchi zenye vita kama Ukraine.

Inabainishwa kuwa orodha ya wasafirishaji wakuwa wa silaha duniani haijabadilika, Marekani ikiongoza kwa kusafirisha asilimia 40 ya silaha duniani ikifuatia Russia, Ufaransa, China na Ujerumani.

**DW**




Balozi wa Ufaransa katika Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa, Nicolas de Rivière (wa pili kushoto) akiwasili na Balozi wa Gabon, Michel Obiang (wa pili kulia), Goma juzi kujadili mzozo wa DRC. **PICHA: AFP**

# ISW: Russia 'haisongi' mbele Bakhmut

**MASCOW,** RUSSIA

TAASISI ya Utafiti wa Vita (ISW) yenye makao yake makuu Mjini Washington nchini Marekani imesema kwamba maendeleo ya Russia yanaonekana kukwama katika kampeni ya Moscow ya kuuteka mji wa Bakhmut mashariki mwa Ukraine.

Taasisi hiyo iliyabainisha hayo mwishoni mwa juma lililopita, ikieleza kwamba hakukuwa na maendeleo yoyote yaliyothibitishwa na vikosi vya Russia huko Bakhmut.

Tathmini ya hivi karibuni ya taasisi hiyo ya wasomi kuhusu vita vya muda mrefu zaidi vya ardhini, ilisema kwamba vikosi vya Russia na vitengo vya Kundi la Wagner linalodhibitiwa na Kremlin viliendelea kufanya mashambulizi ya ardhini katika mji huo lakini hakuna ushahidi kwamba walikuwa wamesonga mbele.

Aidha, Kamanda wa Vikosi vya Ardhini vya Ukraine, Alexander Syrsky, alieleza kuwa mamluki kutoka kundi la Wagner wanakaribia kuuteka mji wa Bakhmut kupitia kila upande, wakijaribu kuvunja ulinzi wa wanajeshi wa Ukraine na kusonga mbele hadi wilaya za kati za jiji.

"Wakati wa vita vikali watetezi wetu husababisha madhara makubwa kwa adui, majaribio yote ya adui kuliteka jiji yanazuiwa na mizinga, vifaru na silaha zingine kali," alisema.

Kwa mujibu wa taasisi ya Marekani ya utafiti wa vita, hadi Machi 8, wanajeshi wa Russia walidhibiti karibu asilimia 50 ya eneo la Bakhmut, mkoa wa Donetsk.

**VOA/BBC**

# MASHABIKI 42 BETIKA MTOKO KIBINGWA KUISHUHUDIA DABI

**Na Mwandishi Wetu**

WAKATI homa ya mechi ya watani wa jadi, Simba na Yanga ikipanda, washindi 42 wa 'Betika Mtoko wa Kibingwa' wamejihakikishia kuishuhudia dabi hiyo laivu hapo Aprili 16, mwaka huu.

Washindi hao ni kati ya 100 watakaopatikana kwenye msimu wa tano wa promosheni hiyo inayoendeshwa na Kampuni ya Michezo ya Kubashiri ya Betika Tanzania.

Ofisa Habari wa Betika, Juvelinaus Rugambwa, alisema bado fursa ipo kwa washindi wengine 58 ambao watabashiri na Betika.

"Bila kujali kama mkeka utachanika au la, kila atakayebashiri nasi ataingia kwenye droo ya Mtoko wa Kibingwa yenye kaulimbiu ya haina mbambamba," alisema.

Alisema mabingwa 42 tayari wamepatikana kutoka mikoa tofauti nchini.

"Wale wa mikoani wamekabidhiwa tayari tiketi zao za ndege kuja Dar es Salaam kuishuhudia laivu dabi hii kwenye Uwanja wa Mkapa," alisema.

Alisema wale wa Dar es Salaam wamefanyiwa usajili na wote kwa pamoja watakutana siku moja kabla ya dabi hiyo ambapo watalala kwenye hoteli ya nyota tano.

"Siku ya mechi watasindikizwa uwanjani kwa king'ora na kukaa vip kutizama dabi hiyo, kwa gharama za Betika," alisema na kuongeza.

"Washindi wanapatikana kupitia droo za kila wiki na kila wiki Betika inatangaza washindi zaidi ya 10, washindi wapya wa wiki hii watatangazwa kesho, keshokutwa na Ijumaa."

Ili kushinda, Rugambwa alisema ni kubeti mikeka mitano kila siku ya kuanzia Sh. 500 na kuendelea.

"Unaweza pia kubeti kwenye website yetu ya www.betika.co.tz au ukapiga *149*16#, mkeka wako uchanike au usichanike moja kwa moja unaingia kwenye droo ya Mtoko wa Kibingwa.

Kwa Dar es Salaam washindi waliofanyiwa usajili ni Norbert Ngangala kutoka Mbezi Luis, Fadiga Samuel wa Ununio, Agogo Ramadhani wa Kigamboni na Hamis Saidi wa Gongolamboto.

**WAVU...**



Mchezaji wa timu ya mpira wa Wavu ya Kampala, Jovi Ngilwa, akiucheza mpira dhidi ya wachezaji wa Wazo katika michuano ya Ligi ya Mkoa wa Dar es Salaam inayoendelea Uwanja wa Ndani wa Mkapa. Kampala ilishinda 3-0. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Polisi Tanzania sasa yapumulia mashine

**Na Adam Fungamwango**

HALI ni mbaya kwa timu ya Polisi Tanzania kutokana na mwenendo wake kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara kutoridhisha, baada ya juzi tena kupata kipigo cha mabao 2-1 dhidi ya Dodoma Jiji.

Yalikuwa ni mabao ya Seif Karihe na Collins Opare yaliyofanya Dodoma Jiji kupanda hadi nafasi ya 11 ya msimamo wa ligi ikifikisha pointi 27, ikiwa kwenye kampeni kabambe ya kuhakikisha inaepuka jinamizi ya kushuka daraja.

Lakini hali ni tofauti kwa Polisi Tanzania ambayo bao lake la kufutia machozi likifungwa na Hilika Hamadi, kwa sasa inaburuza mkia ikiwa na pointi 19, ikibakisha mechi tano tu kabla ya kutamatika kwa Ligi Kuu Tanzania Bara msimu huu.

Kocha Mkuu wa Polisi Tanzania, Mwinyi Zahera, baada ya kumalizika mechi hiyo kwenye Uwanja wa Jamhuri jijini Dodoma, aliwalaumu waamuzi wa mchezo huo kwa madai walionekana kuwabeba wapinzani wao.

"Siwalaumu wachezaji wangu, timu haikucheza vibaya, wamejitolea, lakini namna mpira unavyochezeshwa unashangaa, uamuzi haukuwa mzuri, ilionekana kama leo tulitakiwa tufungwe.

"Kuna makosa ya timu nzima na makosa ya mtu mmoja mmoja, sisi tumeruhusu mabao kwa makosa ya mtu mmoja mmoja, ambayo kwa hali ya kawaida kwa kocha yeyote duniani ni ngumu kuyarekebisha kuliko makosa ya mfumo mzima wa timu," alisema Zahera.

Hata hivyo, alisema yeye atakuwa mtu wa mwisho kuamini kuwa Polisi Tanzania itashuka daraja.

Kwa upande wa Kocha Msaidizi wa Dodoma Jiji, Kassim Liogope, alisema Polisi Tanzania hawakutarajia kukiona walichokiona, kwani waliwabadilishia mfumo, ikawa ni 'sapraizi' kwao.

"Mechi ya leo hatukutaka kuweka chini, Polisi Tanzania asili yao kucheza mpira wa nguvu, sasa mechi hii na sisi tukaona tuingie hivyo hivyo kama wao, 'tukawasapraizi', tukawaweka na mastraika wenye nguvu mbele, wao walijiandaa kucheza na Dodoma Jiji ile ambayo inaweka mpira chini, kwa hiyo tukawapoteza," alisema Liogope.

## Irada Style yaja na jukwaa la mavazi

**Na Moshi Lusonzo**

KAMPUNI ya ubunifu wa mavazi ya Irada Style, imeandaa jukwaa la mavazi ya stara katika kuadhimisha wiki ya Siku ya Wanawake Duniani.

Mkurugenzi wa kampuni hiyo, Irada Mtonga, amesema maonyesho hayo ya mavazi, yatafanyika Ijumaa wiki hii katika Hoteli ya Hyatt Regency jijini Dar es Salaam.

Alisema, pia kutakuwapo na kongamano litakalowakutanisha wanawake kutoka nyanja mbalimbali ikiwamo sanaa, burudani, wanasiasa, wachumi, wafanyabiashara na madaktari.

"Lengo la kuandaa kongamano hili litakaloambatana na maonyesho ya mavazi ni kuwapa wanawake uelewa namna ya uvaaji wa kistaarabu pamoja na kubadilishana uzoefu katika sekta mbalimbali," alisema Irada.

Alisema Irada Style imekuwa lebo kubwa ya mavazi nchini katika kipindi cha miaka mitano na imeleta hamasa kwa wanawake wengi kupenda kuvaa mavazi ya stara ambayo hayakiuki maadili ya Kitanzania.

## Generation Queens mabingwa Ligi Z'bar

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

TIMU ya New Generation Queens imetwaa ubingwa wa Ligi Kuu ya Wanawake Zanzibar baada ya kuifunga UMZ mabao 3-1 katika mchezo wa mwisho wa kukamilisha msimu wa ligi hiyo.

Katika mchezo huo New Generation ilihitaji kushinda au sare ya aina yoyote ili kumzuia mpinzani wake, Warriors Queens, ambaye amemaliza ligi akiwa na alama 28 huku mabingwa hao wakiwa na pointi 30.

New Generation inakuwa timu ya kwanza kutwaa ubingwa mara mbili tangu kuanza kuchezwa ligi hiyo ambayo huu ni msimu wa tatu tangu ianzishwe.

Akizungumza na gazeti hili jana Kocha Msaidizi wa timu hiyo, Ahmad Bakari, alisema hakika msimu huu wamefanikisha walichokihitaji baada ya kushindwa kufanya hivyo msimu uliopita.

Alisema ligi ya msimu huu ilikuwa ngumu kwa kuwa kila timu ilijiimarisha katika mzunguko wa pili kwa kufanya usajili wa wachezaji nje ya Zanzibar.

Kwa kutwaa ubingwa huo, New Generation Queens, itaiwakilisha Zanzibar katika michuano ya Klabu Bingwa Afrika inayoanzia ngazi ya CECAFA.

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### LUKAKU ATAKA KUBAKI
MSHAMBULIAJI wa Ubelgiji, Romelu Lukaku, anataka kubakia Inter Milan mkopo wake utakapoisha, lakini klabu hiyo ya Italia haiwezi kumudu mshahara wa sasa wa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 29. ***(Mail)***

### OSIMHEN AWINDWA PSG
KLABU ya Paris St-Germain imeungana na Chelsea na Manchester United katika harakati za kumsajili mshambuliaji wa Nigeria, Victor Osimhen, mwenye umri wa miaka 24 kutoka Napoli. ***(Nicolo Schira)***

### RAPHINHA AWANIWA CHELSEA
CHELSEA na Newcastle wanafuatilia hali ya Raphinha kule Barcelona kwani klabu hiyo ya Hispania inaweza kuwa tayari kumuuza winga huyo wa Brazil mwenye umri wa miaka 26**. *(Sport)***

### PALHINHA AGOMBEWA EPL
KLABU ya Manchester United inaangalia uwezekano wa kumnunua Joao Palhinha wa Fulham kipindi cha majira ya joto, ingawa Arsenal, Chelsea, Liverpool, Newcastle na Tottenham Hotspur pia zinamfuatilia kiungo huyo wa Ureno mwenye umri wa miaka 27. ***(Sun)***

### ROQUE HAITAKI ARSENAL
VITOR Roque amepinga uwezekano wa kuhamia Arsenal huku mshambuliaji huyo wa Brazil mwenye umri wa miaka 18, akipendelea kuhamia Barcelona kutoka Athletico Paranaense. ***(Sport)***

### CHILWELL AIVUTIA CITY
MANCHESTER City inavutiwa na beki wa kushoto wa Chelsea, Ben Chilwell mwenye umri wa miaka 26. ***(Athletic)***

### JESSE KUTOPEWA MKATABA
KLABU ya Nottingham Forest haiko tayari kumpa mkataba mpya mshambuliaji wa England, Jesse Lingard, 30. ***(Football Insider)***

### LINDELOF ATAKIWA INTER
KLABU ya Inter Milan itajaribu tena kumsajili Victor Lindelof kutoka Manchester United msimu wa majira ya joto baada ya kushindwa kuafikiana kwa mkopo dirisha la Januari na beki huyo wa Sweden mwenye umri wa miaka 28**. *(Sun)***

### THURAM AWANIWA INTER
INTER Milan wanaangalia uwezekano wa kumsajili mshambuliaji wa Ufaransa, Marcus Thuram, mwenye umri wa miaka 25, kutoka Borussia Monchengladbach, licha ya Juventus, Manchester United na Newcastle United kumuwinda. ***(Calciomercato)***

### DIABY ANYATIWA ARSENAL
ARSENAL imekuwa ikimnyatia winga wa Ufaransa, Moussa Diaby, mwenye umri wa miaka 23, kutoka Bayer Leverkusen, lakini huenda pia Newcastle United na Paris St-Germain zinamtaka. ***(Fabrizio Romano)***

### FIRMINO ATAKIWA ATLETICO
KLABU ya Atletico Madrid imejitokeza kuwania saini ya mshambuliaji wa Brazil, Roberto Firmino, mwenye umri wa miaka 31, kama mchezaji huru wakati mkataba wake wa Liverpool utakapokamilika msimu huu wa majira ya joto. ***(Mundo Deportivo)***

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# ARTETA: JESUS ANATAKIWA KUPIGANIA NAMBA YAKE

●●● Tulishazoea kucheza bila yeye, lakini ujio wake una maana kubwa kwetu, lazima apambane...

**LONDON, England**

GABRIEL Jesus amempa Mikel Arteta "wakati mgumu" baada ya fowadi huyo wa Arsenal kurejea kutoka kwenye majeraha katika ushindi wa mabao 3-0 dhidi ya Fulham Jumapili.

Arteta alishaanza kuzoea kumkosa Jesus baada ya kupata jeraha wakati akiwa kwenye majukumu ya Timu ya Taifa ya Brazil wakati wa Kombe la Dunia mwaka jana.

Bado hakuna kosa kwamba Jesus ana jukumu la kucheza wakati huu Arsenal wakipambania kutwaa taji la Ligi Kuu England, lakini Arteta, licha ya kufurahishwa na kurejea kwa mchezaji huyo aliyenunuliwa kwa pauni milioni 45, alisema nyota huyo mwenye umri wa miaka miaka 25," anahitaji kupambania nafasi yake.

Arteta alimuingiza Jesus dakika ya 77 pale kwenye dimba la Craven Cottage akichukua nafasi ya Leandro Trossard, ambaye asisti zake tatu za kipindi cha kwanza zilifungua njia kwa ushindi huo wa dabi ya London.

"Hatukujua kama ulikuwa mchezo sahihi kwake leo (juzi)," alisema Arteta.

"Siku chache zilizopita, aliniambia kuna kitu anakosa, na jana yake akanitazama machoni na kuniambia yuko tayari.

"Leo (juzi) tulipata nafasi ya kumtupa ndani kwa sababu ni hatua ya kwanza ya kumpa nguvu. Alionekana huru na alitengeneza nafasi mbili kubwa mara moja, na ni vizuri kumpata tena.

"Sasa anahitaji kupata nafasi yake kama mtu mwingine yeyote kwenye timu. Tuna njia mbadala ambazo zinaweza kucheza katika nafasi tofauti na tuna majukumu tofauti ya kujaza kuhusiana na kemia ya wachezaji na kile tunachowaomba.

"Nilifurahi sana. Aliweka mengi katika miezi michache iliyopita na sasa amerudi anatakiwa kupambana kupata nafasi yake.

"Tulishaanza kuzoea kucheza bila yeye, lakini ujio wake una maana kubwa sana kwetu, hivyo lazima apambane."

Ushindi huo ulimfanya Arteta kushinda mechi 100 kama kocha wa Arsenal, na nahodha huyo wa zamani wa klabu hiyo, alisema: "Tunatumai kutakuwa na nyingi zaidi."

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!

SUPA JACKPOT KWA 1000/- 1,090,5

JACKPOT MECHI WIKI HII

TAREHE: 14,15 NA 16 MACHI 2023

BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE 13

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 14/03/23 | 23:00 | Porto vs Inter | 2.60 | 3.30 | 2.49 |
| 02. 15/03/23 | 02:05 | Tlaxcala FC vs Venados FC | 2.58 | 3.15 | 2.53 |
| 03. 15/03/23 | 04:10 | Independiente Santa Fe vs America De Cali | 2.27 | 3.06 | 3.01 |
| 04. 15/03/23 | 06:05 | Correcaminos Uat vs Tepatitlan FC | 2.24 | 3.11 | 3.01 |
| 05. 15/03/23 | 19:30 | NK Celje vs Olimpija Ljubljana | 2.62 | 3.23 | 2.39 |
| 06. 15/03/23 | 22:30 | Southampton vs Brentford | 2.85 | 3.15 | 2.38 |
| 07. 15/03/23 | 23:00 | Real Madrid vs Liverpool | 2.33 | 3.46 | 2.68 |
| 08. 16/03/23 | 20:45 | Fenerbahce vs Sevilla FC | 2.23 | 3.37 | 3.16 |
| 09. 16/03/23 | 20:45 | Djurgardens IF vs Lech Poznan | 2.46 | 3.27 | 2.72 |
| 10. 16/03/23 | 20:45 | Slovan Bratislava vs FC Basel | 2.47 | 3.23 | 2.73 |
| 11. 16/03/23 | 23:00 | AZ Alkmaar vs Lazio | 2.83 | 3.28 | 2.37 |
| 12. 16/03/23 | 23:00 | Union Saint Gilloise vs Union Berlin | 2.77 | 3.32 | 2.39 |
| 13. 16/03/23 | 23:00 | Real Sociedad vs Roma | 2.19 | 3.27 | 3.32 |

KUWEKA PESA:
- PIGA *150*87#, CHAGUA 4
- WEKA PESA.

tigo pesa · vodacom m-pesa · halopesa · airtel money

SEND

SportPesa

SPORTPESA.CO.TZ

PIGA *150*87#

GBT:0249 18+ HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA: 0764115588, 0677115588 0685115588

@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# TEN HAG ALIA NA MWAMUZI, KADI NYEKUNDU



**MANCHESTER, England**

ERIK ten Hag alisikitika kwa kukosa uthabiti katika maamuzi ya waamuzi baada ya kuchoshwa na uchezeshaji wa Anthony Taylor kwenye suluhu ya Manchester United na Southampton, Jumapili.

United waliambulia sare hiyo kwenye Uwanja wa Old Trafford baada ya Casemiro kuonyeshwa kadi nyekundu ya moja kwa moja katika kipindi cha kwanza - kutokana na Mbrazil huyo kumfanyia faulo mbaya, Carlos Alcaraz.

Awali, mwamuzi Taylor alimwonyesha Casemiro kadi ya njano, lakini baada ya kupitia ukaguzi wa VAR akaifuta kadi hiyo na kumwonesha nyekundu ya moja kwa moja.

Ina maana Casemiro ndiye mchezaji wa kwanza wa United kupokea kadi mbili nyekundu katika msimu mmoja wa Ligi Kuu tangu Nemanja Vidic msimu wa 2013-14, na atatumikia adhabu ya kufungiwa mechi nne badala ya tatu kwa sababu ni mara ya pili ndani ya msimu mmoja.

"Ninachofikiria ni kutokwenda sawa; wachezaji hawajui tena sera ni nini, na nadhani yote ni katika kila mashindano," alisema Ten Hag akiwaambia waandishi wa habari.

"Tuliona kwenye mchezo wa Leicester na Chelsea hakukuwa na VAR, lakini kwetu ilikuwapo.

"Tulipaswa kupata penalti, hasa ile ya kwanza kwani ilikuwa ya wazi na ya wazi ya mpira wa mikono, kwa hiyo sera ni nini?"

"Ni kweli, tunazungumza, lakini si mengi, kwa hiyo baadhi ya maswali bado tunayo," aliendelea.

"Na ninakuambia: Casemiro ni mchezaji wa haki. Casemiro amecheza mechi zote za Ulaya, zaidi ya 500 hakuwahi kuwa na kadi nyekundu (ya moja kwa moja). Sasa ana mbili.

"Fikiria hilo. Anacheza, lakini anacheza kwa haki. Na pia katika hili, anacheza kwa haki, sawa na dhidi ya Crystal Palace, kwa hivyo inajadiliwa sana."

# Xavi: Ushindi kwa Athletic ni wa dhahabu

**BARCELONA, Hispania**

XAVI alitangaza ushindi mwembamba wa bao 1-0 wa Barcelona dhidi ya Athletic Bilbao kama "ushindi wa dhahabu" baada ya kunusurika na mashambulizi ya dakika tisa na kurejesha uongozi wao wa pointi tisa kabla ya Clasico wikendi ijayo.

Bao la kipindi cha kwanza la Raphinha katika Uwanja wa San Mames, hatimaye lilithibitika kuwa muhimu, lakini hiyo ilikuwa ncha ya barafu kwani Barca walilazimishwa kustahimili shinikizo la dakika za mwisho.

Hapo awali, Raul Garcia alikuwa amegonga nguzo ya wenyeji na Athletic walidhani walipata sare ya kushangaza wakati Inaki Williams alipofunga bao dakika za mwisho, lakini lilikataliwa baada ya ukaguzi wa VAR.



Ulikuwa ushindi muhimu huku Barca wakitarajiwa kukabiliana na Real Madrid walio nafasi ya pili kwenye Uwanja wa Camp Nou, Jumapili.

"Jambo kama hilo limetokea kwetu tena," alisema Xavi akiwaambia waandishi wa habari.

"Tumekuwa kwenye kiwango kizuri kwa dakika 75, ingawa tunapaswa kushambulia zaidi.

"Ulikuwa mchezo mgumu. Hapa San Mames unaishia kuteseka, na ndivyo ilivyotokea. Ni ushindi wa dhahabu kwetu na tunachukua pointi tatu muhimu sana.

"Tulidumisha uongozi wa pointi tisa, na tunaingia Clasico kwa kujiamini.

"Lakini lazima tufanye mashambulizi vizuri zaidi. Tulipata nafasi mbili au tatu za wazi katika kipindi cha pili: kutoka kwa Ansu (Fati); (Alejandro) Balde na (Robert) Lewandowski.

"Tunapaswa kuimarika katika kipengele hicho, kuwa watulivu na wavumilivu zaidi na kucheza zaidi katika kipindi cha ushambuliaji. Uimara wa ulinzi lazima pia uthaminiwe, lakini ni kweli kwamba tunapaswa kuboresha safu ya ushambuliaji."

583,531/-

SUPA JACKPOT
MECHI WIKI HII
BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01.18/03/23 | 18:00 | Aberdeen FC vs Heart of Midlothian FC | 2.38 | 3.40 | 2.65 |
| 02.18/03/23 | 18:00 | Rotherham United vs Cardiff City | 2.55 | 3.15 | 2.65 |
| 03.18/03/23 | 18:00 | Stoke City vs Norwich City | 2.65 | 3.15 | 2.55 |
| 04.18/03/23 | 18:15 | Albacete Balompie vs Granada CF | 2.55 | 2.95 | 2.80 |
| 05.18/03/23 | 18:30 | Portimonense SC vs FC Vizela | 2.75 | 3.05 | 2.50 |
| 06.18/03/23 | 20:30 | Espanyol Barcelona vs RC Celta de Vigo | 2.75 | 3.05 | 2.50 |
| 07.18/03/23 | 20:45 | FC Emmen vs Sparta Rotterdam | 2.50 | 3.10 | 2.70 |
| 08.18/03/23 | 21:00 | Quevilly-Rouen Metropole vs FC Metz | 2.60 | 2.95 | 2.75 |
| 09.18/03/23 | 21:00 | Chamois Niort FC vs Stade Lavallois MFC | 2.60 | 3.00 | 2.70 |
| 10.19/03/23 | 14:15 | FC Groningen vs SC Heerenveen | 2.70 | 3.20 | 2.46 |
| 11.19/03/23 | 14:30 | Sampdoria Genoa vs Hellas Verona | 2.85 | 3.00 | 2.48 |
| 12.19/03/23 | 15:30 | Eintracht Braunschweig vs Hannover 96 | 2.46 | 3.30 | 2.65 |
| 13.19/03/23 | 16:30 | Excelsior Rotterdam vs SC Cambuur | 2.55 | 3.30 | 2.50 |
| 14.19/03/23 | 17:00 | ESTAC Troyes vs Stade Brest 29 | 2.70 | 3.20 | 2.45 |
| 15.19/03/23 | 18:15 | CA Osasuna vs Villarreal CF | 2.90 | 3.05 | 2.40 |
| 16.19/03/23 | 19:00 | FK Austria Wien vs SK Rapid Wien | 2.40 | 3.15 | 2.45 |
| 17.19/03/23 | 20:00 | Lazio Rome vs AS Roma | 2.60 | 2.95 | 2.75 |

MECHI ZA USHINDI
"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE "2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

JUMANNE - 14/03/2023

| MUDA | GAME ID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 14:45 | 2723 | Balestier Khalsa vs Tampines | 3.79 | 4.30 | 1.63 |
| 16:00 | 1575 | Kairat Almaty vs FK Kaspiy Aktau | 1.50 | 3.94 | 5.33 |
| 16:00 | 3754 | Tobol Kostanay vs Shakhter Karagandy | 1.42 | 4.09 | 6.14 |
| 16:00 | 5211 | Ethiopian Medhin vs Arba Minch Kenema | 2.20 | 2.95 | 2.90 |
| 16:00 | 5950 | Ordabasy vs FC Zhetysu | 1.39 | 3.80 | 6.40 |
| 16:15 | 4143 | Al Wehda vs AL Baten | 1.68 | 3.69 | 4.26 |
| 16:30 | 3900 | Platinum City Rovers vs Mm Platinum FC | 2.15 | 2.78 | 3.50 |
| 16:30 | 5468 | Ajax Cape Town vs Baroka FC | 1.97 | 3.02 | 3.69 |
| 17:30 | 3684 | Akron Tolyatti vs Lokomotiv Moscow | 3.63 | 3.37 | 1.90 |
| 17:35 | 1793 | Al Suwaiq vs Al Nahda (Oman) | 3.00 | 2.69 | 2.53 |
| 18:00 | 2935 | Kaisar Kyzylorda vs Aksu | 2.38 | 3.24 | 2.62 |
| 18:00 | 3070 | Astana vs Aktobe | 1.43 | 4.11 | 5.97 |
| 18:05 | 3912 | AL Sahel SC vs AL Qaisoma | 2.33 | 2.81 | 3.07 |
| 20:00 | 1029 | Spartak Moscow vs Ural Yekaterinburg | 1.69 | 3.77 | 4.14 |
| 20:00 | 1148 | Alessandria vs Fermana FC | 2.63 | 2.87 | 2.93 |
| 20:30 | 4565 | Mamelodi Sundowns vs Bloemfontein Celtic | 1.44 | 4.09 | 6.71 |
| 20:30 | 5451 | Cape Town City vs Marumo Gallants FC | 2.10 | 2.93 | 3.66 |
| 21:00 | 1477 | Paris FC vs Amiens | 2.03 | 3.25 | 3.45 |
| 21:00 | 2965 | Hallescher vs Viktoria Koln | 2.34 | 3.32 | 2.85 |
| 21:00 | 3257 | 1860 Munich vs SV Elversberg | 3.22 | 3.38 | 2.11 |
| 21:00 | 3280 | Meppen vs Verl | 2.79 | 3.37 | 2.36 |
| 21:00 | 5287 | RW Essen vs Osnabruck | 3.05 | 3.37 | 2.20 |
| 21:00 | 5440 | Zwickau vs Erzgebirge Aue | 2.91 | 3.23 | 2.35 |
| 22:45 | 1450 | Stevenage vs Crewe | 1.34 | 4.46 | 7.74 |
| 22:45 | 1819 | York City vs Altrincham | 2.33 | 3.24 | 2.88 |
| 22:45 | 2635 | Sutton United vs Grimsby | 1.99 | 3.18 | 3.52 |
| 22:45 | 2689 | Wigan vs Coventry | 2.70 | 3.15 | 2.48 |
| 22:45 | 2852 | Halifax vs Bromley | 2.23 | 3.25 | 3.04 |
| 22:45 | 2911 | Blackpool vs QPR | 2.54 | 3.14 | 2.64 |
| 22:45 | 2999 | Wealdstone vs Chesterfield | 4.42 | 3.63 | 1.71 |
| 22:45 | 3162 | Maidenhead U vs Aldershot | 2.23 | 3.25 | 3.04 |
| 22:45 | 3203 | Solihull Moors vs Scunthorpe | 1.79 | 3.63 | 4.00 |
| 22:45 | 3317 | Barnet vs Yeovil | 1.77 | 3.63 | 4.10 |
| 22:45 | 3739 | Burton vs Peterborough | 3.13 | 3.53 | 2.10 |
| 22:45 | 3783 | Bristol Rovers vs Wycombe | 2.73 | 3.39 | 2.39 |
| 22:45 | 3985 | Southport vs Boston Utd | 2.43 | 3.22 | 2.65 |
| 22:45 | 3996 | Newport vs AFC Wimbledon | 2.05 | 3.13 | 3.43 |
| 22:45 | 4295 | Rotherham vs Preston | 2.47 | 3.05 | 2.80 |
| 22:45 | 4311 | Northampton vs Mansfield | 2.16 | 3.11 | 3.16 |
| 22:45 | 4333 | Millwall vs Swansea | 1.89 | 3.35 | 3.80 |
| 22:45 | 4504 | Morecambe vs Charlton | 3.12 | 3.38 | 2.16 |
| 22:45 | 4682 | Boreham Wood vs Southend | 2.31 | 3.15 | 2.99 |
| 22:45 | 4926 | Watford vs Birmingham | 1.82 | 3.39 | 4.09 |
| 22:45 | 4941 | Weymouth vs Hungerford Town | 2.15 | 3.32 | 3.01 |
| 22:45 | 5178 | Walsall vs Swindon Town | 2.22 | 3.08 | 3.08 |
| 22:45 | 5396 | Notts County vs Eastleigh | 1.33 | 4.84 | 8.00 |
| 22:45 | 5403 | Accrington vs Portsmouth | 3.38 | 3.43 | 2.03 |
| 23:00 | 2206 | Manchester City vs RB Leipzig | 1.39 | 4.55 | 6.68 |
| 23:00 | 2417 | Middlesbrough vs Stoke City | 1.81 | 3.49 | 3.99 |
| 23:00 | 2955 | Porto vs Inter | 2.55 | 3.26 | 2.55 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# JKT TANZANIA YABISHA HODI LIGI KUU 2023/24

**Na Adam Fungamwango**

NI kama vile maafande wa JKT Tanzania wanahesabu siku tu kuweza kupanda daraja na kucheza Ligi Kuu Tanzania Bara kutokana na kuendelea kuzinyanyasa timu za Ligi ya Championship, juzi ikiwa ni zamu ya maafande wenzao wa Green Warriors walipoibamiza mabao 3-1, mechi ikichezwa Uwanja wa Uhuru, Dar es Salaam.

Ni ushindi unaowaweka sehemu nzuri ya kucheza Ligi Kuu Tanzania Bara kwa msimu wa 2023/24, ikiendelea kushikilia usukani wa Ligi ya Championship, ikiwa na pointi 53, ikicheza mechi 21, kushinda 17, sare mbili na kupoteza mbili, ikibakisha mechi tisa tu kumaliza mechi zake msimu huu.

Mabao ya washindi yalifungwa na Edward Songo dakika ya 10, Elia Ashley dakika 72 na Mohamed Bakari dakika ya 83.

JKT Tanzania inaongoza ligi hiyo kwa tofauti ya pointi 11, juu ya Kitayosce ambayo inashika nafasi ya pili kwa pointi 42 mpaka sasa.

Matokeo ya mechi zingine, Biashara United ililazimishwa suluhu kwenye uwanja wake wa nyumbani wa Karume, Musoma mkoani Mara dhidi ya Mbuni FC.

Matokeo hayo yanaifanya Biashara kuwa kwenye nafasi ya tisa kwa pointi 26, Mbuni ikiwa ya nane ikifikisha pointi 30.

Kwenye Uwanja wa Nelson Mandela, Sumbawanga mkoani Rukwa, KenGold iliichapa Mashujaa mabao 2-1, ikiifanya kufikisha pointi 33 kwenye nafasi ya sita, Mashujaa wakisalia kwenye nafasi ya tano na pointi zao 35.

Kwenye Uwanja wa Nangwanda Sijaona Mtwara, wenyeji Ndanda walikiona cha moto kwa kutandikwa mabao 3-1 dhidi ya Fountaine Gate.

Hali si nzuri kwa Ndanda, kwani ina pointi 13 tu ikiwa nafasi ya 15 na kama itaendelea na mwenendo huo inaweza kushuka daraja kwenda Ligi Daraja la Pili.

Copco nayo iliidungua African Sports bao 1-0 kwenye Uwanja wa CCM Kirumba jijini Mwanza.



Kipa wa Timu ya Green Warriors, Fahad Idrisa (kushoto), akiokoa hatari kwa kuucheza mpira wa kichwa uliopigwa na mchezaji wa timu ya JKT Tanzania katika mchezo wa Ligi ya Championship uliochezwa Uwanja wa Uhuru, Dar es Salaam juzi. JKT Tanzania ilishinda mabao 3-1. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Simba, Yanga mawindoni CAF

INATOKA UK. 24

Chamazi ni bure, ni kwa sababu hawana na wao wanafanya kuvutia watu waende uwanjani, lakini Simba tunao mashabiki, tena wenye uwezo wa kuamua kwenda uwanjani na si lazima kuwafanyia bure, wana uwezo wa kwenda uwanjani kwa kiingilio kwa hiyo wanatakiwa wajitokeze kwa wingi Jumamosi."

Kwa upande wa Yanga, Kocha Mkuu wa timu hiyo, Nesreddine Nabi, naye ameanza mapema maandalizi ya mchezo wao wa Kombe la Shirikisho Afrika dhidi ya US Monastir, ambapo amesema anahitaji washambuliaji kusaka matokeo mapema kwa kuongeza nguvu ya kujiamini na kucheza kwa utulivu hasa dakika za mwanzo za mchezo.

Akizungumza na gazeti hili jana, Nabi aliwasifia wachezaji wake kucheza vizuri dhidi ya Geita Gold FC, lakini ameona madhaifu katika mchezo huo ikiwa ni pamoja na safu ya ushambuliaji kutotafuta matokeo ya mapema. "Tunakutana na timu imara, na lazima tunahitaji matokeo, tunapaswa kufanya kazi kubwa kwenye kutumia nafasi za mwanzo zitakazotufanya tuwe imara na kupata matokeo mazuri, hii si mechi ya ligi bali tunahitaji ushindi," alisema Nabi.

Alisema US Monastir wako imara, na wana wachezaji wazuri ingawa hata wa Yanga ni wazuri lakini suala la kutumia nafasi wanazotengeneza bado ni tatizo kwao.

Nabi alisema wanarejea katika uwanja wa mazoezi kufanyia kazi madhaifu yaliyojitokeza mechi ya Geita Gold FC ambayo walipata ushindi mzuri, ili kuweza kushinda dhidi ya US Monastir.

Endapo Simba na Yanga zitashinda mechi zao hizo, Jumamosi na Jumapili zitakuwa zimefuzu hatua ya robo fainali na hiyo kuwa mara ya kwanza katika historia ya soka la Tanzania kwa miamba hiyo kwa msimu mmoja yote kutinga hatua ya robo fainali.

Michezo

Jumanne Machi 14, 2023

Nipashe



UKURASA 21

## Arteta: Jesus apigania namba yake

UGALI ZAIDI...




Mshambuliaji kinda wa Yanga, Clement Mzize (kushoto), akipimana 'ugali' na beki mkongwe wa Geita Gold FC, Kelvin Yondani, wakati wakiwania mpira kwenye mechi ya Ligi Kuu Bara iliyopigwa Uwanja wa Azam Complex, Dar es Salaam juzi na Yanga kushinda 3-1. **MPIGAPICHA WETU**

# FEI TOTO AITWA STARS MECHI KUFUZU AFCON

● ● ●Kuivaa Uganda akiungana na Samatta, Msuva na mastaa kibao wanaokipiga nje, yumo pia...

**Na Adam Fungamwango**

KIUNGO mshambuliaji Feisal Salum 'Fei Toto', ni miongoni mwa wachezaji 31 walioitwa kwenye kikosi cha Timu ya Taifa ya Tanzania, Taifa Stars kwa ajili ya kujiandaa na mechi mbili dhidi ya Uganda za kusaka nafasi ya kufuzu fainali za AFCON 2024 zitakazofanyika Januari hadi Februari mwakani nchini Ivory Coast.

Fei Toto, ameitwa kwenye timu ya taifa akiwa hayupo kwenye kikosi cha Yanga kinachocheza Ligi Kuu na michuano ya Kombe la Shirikisho barani Afrika, na hivi karibuni akiwa amewasilisha barua kwenye ofisi za Shirikisho la Mpira wa Miguu nchini (TFF), kuomba kuvunja mkataba na klabu yake hiyo.

Awali, Kamati ya Sheria na Hadhi za Wachezaji ya TFF ilitangaza kuwa Fei Toto ni mchezaji halali wa Yanga, baada ya kutokea mgogoro wa kimkataba baina ya pande zote, ulioanza mwishoni mwa mwaka jana.

Mbali na mchezaji huyo, ambaye hajaonekana uwanjani kwa muda mrefu sasa, taarifa iliyotolewa jana na Idara ya Habari na Mawasiliano ya TFF chini ya Cliford Ndimbo, iliwataja wachezaji waliochaguliwa kujiunga na kikosi hicho ni Aishi Manula, Beno Kakolanya, Mzamiru Yassin kutoka Simba, Metacha Mnata, Kibwana Shomari, Fei Toto, Dickson Job, Bakari Mwanyeto, Mudathir Yahaya na Ibrahi Baka kutoka Yanga.

Wengine ni Datius Peter, David Luhende, Anuary Jabir na Abdallah Mfuko kutoka Kagera Sugar, Yahaya Mbegu kutoka Ihefu, Yasuph Kagoma wa Singida Big Stars, Sospeter Bajana na Abdul Suleiman 'Sopu' wa Azam FC, Edmund John wa Geita Gold, na Khalid Habibu wa KMKM.

Wachezaji wa Kitanzania walioitwa wanaosakata soka la kulipwa nje ya nchi ni pamoja na nahodha Mbwana Samatta kutoka KRC Genk ya Ubelgiji, pamoja Kelvin John ambaye anaichezea klabu hiyo, Simon Msuva wa Al-Qadsiah ya Saudi Arabia, Ramadhani Makame wa Bodrumspor ya Uturuki, Novetus Dismas wa Zulte Waregem ya Ubelgiji, Alphonce Mabula wa FK Spartak Subotica ya Serbia, Ben Starkie anayeichezea Basford United FC ya Uingereza, Haji Mnoga wa Aldershot Town ya Uingereza, Ally Msengi wa Swallows ya Afrika Kusini, Himid Mao wa Ghazi El Mahala SC ya Misri na Said Khamis wa Al-Fujairah ya Falme za Kiarabu.

Kikosi hicho kitakuwa chini ya Kocha Mkuu Adel Amrouche raia wa Algeria aliyetangazwa hivi karibuni, na kupewa jukumu la kukinoa kikosi cha Taifa Stars.

## Simba, Yanga mawindoni CAF

**Adam Fungamwango na Saada Akida**

MAPEMA tu baada ya kumaliza majukumu yao ya mechi za Ligi Kuu Bara, Simba ikiirarua Mtibwa Sugar mabao 3-0 Jumamosi iliyopita huku Yanga ikishinda 3-1 dhidi ya Geita Gold FC juzi, miamba hiyo ya soka nchini imeanza maandalizi kuelekea mechi zao za kimataifa mwishoni mwa wiki.

Simba itaikaribisha Horoya AC ya Guinea katika mechi ya Kundi C ya Ligi ya Mabingwa Afrika Jumamosi wiki hii katika Uwanja wa Benjamin Mkapa kabla ya kesho yake, Jumapili Yanga kuvaana na US Monastir ya Tunisia uwanjani hapo kwenye mchezo wa Kundi D wa Kombe la Shirikisho Afrika.

Kuelekea mechi hiyo, Klabu ya Simba imesema haiko tayari kuishia hatua ya makundi kwenye michuano ya Ligi ya Mabingwa inayoendelea, badala yake inataka kutinga robo fainali na kuendelea kama mambo yataenda kama yalivyopangwa.

Meneja Habari na Mawasiliano wa klabu hiyo, Ahmed Ally, amesema kwa sasa timu ya Simba hadhi yake si ya kuishia hatua ya makundi, hivyo kwa namna yoyote ile wamejiandaa kuhakikisha wanatinga hatua ya robo fainali.

"Horoya ni timu nzuri, lakini kama tukiungana, wachezaji, viongozi na mashabiki wale tunawamudu, hawatokuwa na maajabu ya kutushinda, hasa nyumbani kwetu, kwao walitufunga bao moja, lakini shughuli waliiona, sasa wanakuja kwetu na hii ni mechi ya kuamua nani aende na nani abaki. Simba hatuko tayari kubaki makundi. Hatuko tayari kwa namna yoyote ile kuishia hatua ya makundi, kwa miaka ya karibuni sisi siyo timu ya kuishia makundi kwa hali yoyote ile, hadhi yetu ni robo fainali kwanza, baada ya hapo sasa chochote kinaweza kutokea, lakini hatutafika huko na maneno ila kwa vitendo, kila mmoja atimize wajibu wake," alisema Ahmed.

Alisema wanajivunia klabu yao kuwa na wanachama na mashabiki wengi ambao wanajitolea kwa hali na mali, ikiwamo kujazana uwanja kwenda kuwashangilia tofauti na baadhi ya klabu kama Mamelodi Sundowns au Azam zinazohaha kuvutia watu waende viwanjani.

"Leo hii unatazama timu kama Mamelodi Sundowns mechi yao kubwa, lakini kiingilio ni bure, unajua kwa nini? Ni kwa sababu hawana mashabiki, wanafanya kuwavutia watu waende mpirani kwenye mechi zao. Msimu huu tangu ligi imeanza mechi za Azam pale

INAENDELEA UK. 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >